# Nipashe

Jumamosi Februari 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580143

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710





UKURASA 13



## Maofisa TRA kortini madai kujifanya Usalama wa Taifa

UKURASA 3

# Ubunge wa Zitto sasa njia panda



**AITWA** msaliti kuiandikia Benki ya Dunia kuinyima serikali mkopo, Spika amtwika zigo AG...

*Endelea ukurasa wa 2*



## SAA 5 DAKIKA 13 LUGOLA KIKAANGONI TAKUKURU

UKURASA 2

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (katikati), akitoka kuhojiwa katika ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), jijini Dodoma jana. Kushoto ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Meja Jenerali Jacob Kingu akiwasili katika ofisi ya taasisi hiyo, kwa ajili ya kuhojiwa na aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye akiwasili katika ofisi hizo. **PICHA: RENATHA MSUNGU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


## Mwanafunzi auawa akicheza kamari

UKURASA 3


**MICHEZO** SIMBA, COASTAL UNION KIBARUANI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mbunge ataka sheria ya mikopo elimu ifumuliwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Susan Lyimo (Chadema), ameitaka serikali kupeleka bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu utakaokuwa na masharti rahisi kwa wanufaika wa mikopo kurejesha kwa wakati.

Lyimo ambaye ni Waziri Kivuli wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipopewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa wizara hiyo.

Alisema kuwa licha ya serikali kuongeza kiwango cha makato katika mishahara ya wanufaika wa mikopo hiyo kutoka asilimia nane hadi 15, idadi ya waliofanikiwa kumaliza kulipa mikopo yao ni ndogo.

Alibainisha kuwa tangu mwaka 1994 serikali ilipoanza kutoa mikopo hiyo, kati ya wanufaika 500,000, ni 11,000 tu waliorejesha mikopo na kumaliza madeni yao hadi mwaka 2019.

Alisema hali hiyo inachangiwa na kuongezeka kwa asilimia sita ya deni kila mwaka, hivyo kulifanya kuwa deni lisiloisha kirahisi.

"Hapo sheria ilikuwa bado, serikali haioni nyongeza hii kubwa itasababisha wanafunzi badala ya kulipa miaka minne au 10, itaenda hadi miaka na hao wanufaika watakuwa wamefariki au kustaafu?" Alihoji.

Katika majibu yake, Naibu Waziri wa wizara hiyo, William Ole Nasha, alisema baada ya kuingia madarakani mwaka 2015, urejeshaji ulikuwa Sh. bilioni 23 kwa mwaka, lakini baada ya kuweka jitihada mwaka huu wanatarajia kukusanya Sh. bilioni 200.

Alisema mwaka 2019 zilikusanywa Sh. bilioni 183 na kwamba shida siyo kwenye tozo ya kulinda thamani ya fedha (deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka), bali ni watu wenyewe wanaorejesha mikopo.

"Mpango wa kuleta marekebisho ya sheria unaonyesha sheria ya sasa bado inakidhi mahitaji ya utoaji mikopo nchini. Kama mbunge anaona kuna haja ya kuleta mabadiliko ya sheria, hiyo ndio kazi ya Bunge, sisi serikali tunaridhika na sheria ya sasa," alisema.

Waziri Prof. Joyce Ndalichako, pia alisimama na kutoa ufafanuzi kuwa serikali za wanafunzi zinatambulika na kuthaminiwa kwa kuwa ni daraja muhimu kati ya wanafunzi na uongozi wa chuo na wanafunzi.

Aliwataka wanafunzi hao watumie taratibu zinazotakiwa kufikisha malalamiko si kufanya kama wanavyofanya baadhi ya viongozi, ikukumbukwa kuwa hivi karibuni aliagiza kuchukuliwa hatua kwa viongozi wa serikali ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha

INAENDELEA UK. 8

# Ubunge wa Zitto sasa njia panda

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

UBUNGE wa Zitto Kabwe (Kigoma Mjini ACT-Wazalendo) umeingia shakani baada ya kudaiwa msaliti kutokana na kuandika barua Benki ya Dunia kuzuia kuipa serikali mkopo huku Mwanasheria Mkuu wa Serikali akitakiwa kumchunguza kama kuna ukiukwaji wa katiba.

Kutokana na madai hayo, baadhi ya wabunge wametaka achukuliwe hatua stahiki kwa kuinyima serikali fursa ya kupata fedha ambazo zingesaidia kwenye maendeleo ya elimu.

Mjadala juu ya sakata la Zitto ambaye pia ni Kiongozi wa ACT-Wazalendo, liliibuka bungeni baada ya Mbunge wa Siha (CCM), Dk. Godwin Mollel, kuomba bunge lisimamishe shughuli zake ili kujadili suala hilo.

Akijenga hoja yake ili aungwe mkono na wabunge, Dk. Mollel alisema: "Nasimama kwa kanuni ya 47 (1) ili kuomba kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura. Hapa juzi, mwenzetu Zitto ameandika barua Benki ya Dunia akitaka fedha zizuiwe ambazo zingekuja kusaidia elimu Tanzania.

"Lakini pesa hizo zingekuja tungejenga shule tano kubwa kwa kila wilaya, lakini tungeweweka bwenini zaidi ya watoto 2,000 wa kike ambao mwisho wa siku hata kiwango cha mimba kwa taifa letu kingeshuka sana."

Alisema wabunge waliapa Bungeni kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katiba hiyo imetaja dhahiri maadui wa taifa letu ikiwamo umaskini, ujinga na maradhi.

Mollel alisema: "Unapogusa kwenye eneo hilo la elimu ina maana umefuta ujinga, umaskini na maradhi. Lakini kwa sababu amevunja katiba, Bunge linatakiwa kutafuta namna ya kushughulikia tabia hiyo kwenye taifa letu.

"...kama hali hii ikiendelea usalama wa nchi yetu utakuwa hatarini na hata maadui wetu wa kiuchumi watapata fursa ya kutuingilia. Kwa hiyo ninaomba nitoe hoja wabunge wenzangu waniunge mkono. Mbunge mwenzetu anazunguka duniani kuhujumu taifa hili kiuchumi na kuathiri usalama," alisema.

**HOJA YAPINGWA**

Baada ya kuwasilisha hoja yake, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Salome Makamba, alisimama kuomba utaratibu akitumia kanuni ya 48 (4), akisema jambo alilolileta Dk. Mollel, wengine hawana taarifa. Pia alisema jambo hilo lina utaratibu wake mahususi na kwa sababu hiyo kulileta ndani ya Bunge kama hoja ya dharura ni kukiuka kanuni.

"Kwa hiyo kama Dk. Mollel anadhani kwamba mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe amekiuka utaratibu wa kibunge na jambo hili linatakiwa kushughulikiwa, zipo njia za kisheria zinazoweza kushughulikia jambo hilo, hivyo alipeleke kwenye vyombo vya kisheria badala ya kuleta kama hoja ya dharura ndani ya Bunge," alisema.

Baada ya hapo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimruhusu tena Dk. Mollel kulieleza zaidi bunge kwamba kuna uki

INAENDELEA UK. 8



Watumishi wa moja ya kambi za utalii, katika Mji mdogo wa Mto wa Mbu, wakihamisha mahema, baada ya kambi hiyo, kukumbwa na mafuriko yalisababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha, wilayani Monduli mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Saa tano dakika 13 za Lugola Takukuru

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, jana alihojiwa kwa takribaini saa tano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kufuatia agizo la Rais John Magufuli baada ya wizara hiyo kukumbwa na kashfa ya kuingia mkataba wa mabilioni ya shilingi kinyume cha sheria.

Januari 23, mwaka huu, Rais Magufuli alimtumbua Lugola akiwa jukwaani ikiwa ni siku 572 tangu ateuliwe kushika wadhifa huo Julai Mosi mwaka 2018.a

Jana saa 1:24 asubuhi, Lugola aliwasili kwenye ofisi za Makao Makuu ya Ofisi za Takukuru jijini Dodoma na kuhojiwa hadi saa 6:34 mchana alipotoka katika eneo hilo.

Baada ya kuwasili kwenye ofisi hizo, Lugola aliyekuwa amebeba Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisalimiana na waandishi wa habari na kuingia ndani ya ofisi hizo, lakini hakuwa tayari kuzungumza na waandishi wa habari baada ya mahojiano.

Alisema: "Siwezi kuongea chochote kwa siku ya leo (jana) mpaka wakati mwingine."

Mbali na Lugola, Takukuru pia iliwahoji watumishi wengine wawili wa serikali ambao ni aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu.

Baada ya Lugola kuhojiwa, alifuata Meja Jenerali Kingu, ambaye aliwasili katika Ofisi za Takukuru majira ya 10:44 asubuhi akitumia gari aina ya Land Cruiser lenye namba za usajili STL 2763. Aliingia kwenye chumba cha mahojiano saa 6:35 mchana na kutoka saa 8:33 mchana.

Maofisa wa Takukuru baada ya mahojiano na Meja Jenerali Kingu, waligeukia kwa aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Andengenye.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Yusuph Masauni, anatarajiwa kuhojiwa leo pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ramadhan Kailima.

Watumishi hao wanahojiwa kutokana na agizo la Rais Magufuli kuhusu mkataba uliongiwa na Wizara ya

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA

## Mwanafunzi adaiwa kuuawa kwa kisu akicheza kamari

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MWANAFUNZI wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Nkomolo, Nkasi mkoani Rukwa, Fredy Pupa (19), anadaiwa kuuawa kwa kuchomwa kisu wakati akicheza kamari baada ya kudhulumiana fedha na mwenzake katika mchezo huo.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Saidi Mtanda, alisema juzi kuwa tukio hilo lilitokea Januari 29 majira ya saa 11 jioni wakati mwanafunzi huyo akiwa na kijana mwenzake aliyefahamika kwa jina la Samwel Nkoswe (20) wakicheza kamari.

Alisema mtuhumiwa wa mauaji hayo, alikuwa ameacha shule na alikuwa anaishi mtaani, huku akijihusisha na vitendo haramu ikiwamo kucheza kamari na siku hiyo alikuwa akicheza mchezo huo na mwanafunzi huyo ambaye alikuwa rafiki yake.

Wakiwa wanacheza mchezo huo, Mtanda alisema Nkoswe alikula fedha za mwanafunzi huyo, lakini alikataa kumpa pesa hizo, ndipo alipotoa kisu alichokuwa nacho mfukoni na kumchoma Pupa ubavuni karibu na tumboni.

Kwa mujibu wa Mtanda, kitendo kilichosababisha kuvuja damu nyingi na kupoteza maisha muda mfupi baadaye.

Baada ya kuona amefanya tukio hilo, Mtanda alisema Nkoswe alikimbia na kwenda kujificha katika mashamba yaliyopo kijijini hapo lakini wananchi walimsaka mpaka kumkamata na kisha kumpa kipigo kikali na sasa yuko hoi hospitalini akiendelea kupatiwa matibabu.

Alisema polisi walifika eneo la tukio na kuuchukua mwili wa marehemu na kisha kuupeleka kituo cha afya kwa ajili ya kuufanyia uchunguzi na kisha kukabidhiwa kwa ndugu zake na kufanya maziko juzi.

Katika maziko hayo, Mtanda ambaye pia ni mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, alitoa salamu za pole kwa familia iliyompoteza mtoto wao na kuwaonya wanafunzi kutojihusisha na mambo mengine tofauti na masomo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo .



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akijadiliana jambo na Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

## Maofisa TRA kortini madai kujifanya Usalama wa Taifa

**Na Hellen Mwango**

WATU sita wakiwamo maofisa wawili Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na aliyekuwa askari Polisi wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu, kujipatia fedha isivyo halali, kujifanya maofisa Usalama wa Taifa, TRA na kutakatisha Sh. milioni 57.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mkunde Mshanga na Gloria Mwenda.

Mshanga aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Mohamed Abdallah maarufu kama Zungu, Mrisho Hassan, Edgan Foluba (Ofisa Forodha Mwandamizi), Elizabeth Mohamed (Ofisa Forodha Msaidizi), Victor Gama (dereva) na aliyekuwa askari polisi Seleman Lusonzo.

Mshanga alidai kuwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote kwa pamoja katika siku isiyofahamika walipanga na kukubaliana kujipatia Sh. milioni 57 na kujinufaisha.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa Januari 2, mwaka huu, katika eneo la Upanga jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walikula njama na kujipatia fedha kutoka kwa Haroub Abdallah wakimdanganya kuwa watabadilisha fedha haramu iliyobadilishwa kimakosa kwa Kamishna wa Forodha.

Jamhuri ilidai kuwa shtaka la tatu, Januari 2, mwaka huu, Mohamed Abdala na Mrisho Hassan katika eneo la Upanga, walijitambulisha kuwa ni maofisa wa TRA na Usalama wa Taifa huku wakijua ni makosa na kinyume cha sheria.

Shtaka la nne la matumizi mabaya ya madaraka linawakabili mshtakiwa Edgan Foluba, Elizabeth Mohamed na Konstebo Lusonzo ambao kwa pamoja wakiwa watumishi, walijipatia Sh. milioni 57 kutoka kwa Abdallah wakimdanganya kuwa watampeleka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa ahadi ya kumsaidia kubadilisha fedha haramu. Kosa hilo wanadaiwa kulitenda Januari 2, mwaka huu.

Katika shtaka la tano la kutakatisha fedha, washtakiwa wote kwa pamoja katika eneo la Upanga, wanadaiwa walidhamiria na kujipatia Sh. milioni 57 kutoka kwa Abdala wakijua wazi ni zao la fedha zilizopatikana kwa udanganyifu.

Baada ya kusikiliza mashtaka yao, Hakimu Chaungu alisema washtakiwa hawatakiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 13, mwaka huu itakapotajwa. Washtakiwa wamepelekwa mahabusu.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

**Kwa idhini tuliyopewa na Banc ABC, tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wao,ambayo ni Nyumba kama ilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | REVOCATUS FABIAN KIWESI | Nyumba ya makazi/Biashara iliyoko kwenye kiwanja chenye hati na.80 kitalu na.1 hati na.88107 ofisi ya ardhi na.414179 eneo la Ukuni Bagamoyo yenye jina la REVOCATUS FABIAN KIWESI | 22nd FEBRUARY 2020 |

MASHARTI YA MNADA
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: AU

Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE: +255 715-363537/ +255 765-363537

Mkurugezi Mtendaji
Banc ABC
Bib titi Mohamed Road,
P.O.BOX 31
DAR ES SALAAM
Tel:+255 222119422

**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**RE-ADVERTISEMENT**

Under the Instruction from **AFRICAN BANKING CORPORATION (T) LTD (BANC ABC),** we shall sell by public auction the Legal Mortgage Securities Under the derivate rights under the Tanzania --Law, which is Industrial Property. The auction will be conducted from 10:00 A.M where the property is located as indicated in the table below:

| No. | DEBTOR/GUARANTER | LOCATION/DESCRIPTION OF PROPERTY | DATE OF AUCTION |
|---|---|---|---|
| 1 | AGRO FOCUS (T)LTD | INDUSTRIAL PROPERTY LOCATED ON PLOT/FARM 1/1 BLOCK" O"NANGWALA AREA IN NEWALA URBARN WTH C.T.NO.1779 MTW, LO.NO.255747 NEW/9270 WITH PLOT AREA 12.056 HECTERS. | 28th FEBRUARY 2020 |

TERMS AND CONDITION FOR THE AUCTION
1. Once bidder has accepted, he or she has to make payment of 25%of the bid price on the same day of auction .The remaining balance of 75% shall be paid within 14 days of the date of the auction OR as per bank agreement with purchaser.
2. Failure to settle the remaining balance within 14 days or as per bank agreement with purchaser shall result to forfeiture of 25% advance payment and other bidders with financial and technical capacity will be considered and who will comply with condition No.4
3. All expenses and costs in respect of inspecting the property, conducting search, transfer and any other expenses incidental thereof shall be borne by the purchaser.
4. Foreign and Local investors are invited to bid in the public auction but should comply with Tanzania Laws for doing business and Land ownership.

**For more Details Please Contact:**

**Managing Director**
**Banc ABC**
**Head Office,**
**Bibi Titi Mohamed Road**
**P.O.Box 31 Dar es salaam**
**Tel: +255 22 2119422**

**Managing Director ,**
**Best group(T)LTD Head Office ,**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Building ,2nd Floor.**
**P.O.BOX 1088 Dar Es Salaam**
**Mobile: +255 715 363537/+255 765 363537, +255 222112402 Email:Info@bestgroup.co.tz**

215612302

# DC aagiza wazazi kuburuzwa kortini watoto kutoripoti shule

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njuwayo, ameagiza wazazi na walezi 111 kufikishwa mahakamani kwenda kujibu tuhuma za watoto wao kushindwa kuripoti shuleni tangu kufunguliwa.

Njuwayo alitoa agizo hilo juzi akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kuzungumza na walimu, wanafunzi na wazazi kuhusiana na mikakati ya kuinua ufaulu katika wilaya hiyo.

Wazazi walioamriwa kufikishwa mahakamani ni kutoka katika kata za Ikwiriri, Mgomba, Mkongo, Ngorongo na Kipungira.

Alisema wazazi hao ni wa wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni tangu shule zilipofunguliwa Januari 6, mwaka huu, na hakuna taarifa yoyote kwa walimu kuhusiana na utoro wao.

"Nimechoka siwezi kuwa Mkuu wa Wilaya wa shule 10 za mwisho za ufaulu kwa sababu za utoro kisa wazazi wanashindwa kusimamia watoto wao. Nendeni mahakamani mtajibu huko waliko watoto wenu na kwa nini hawaonekani shuleni hadi sasa," alisema.

Aidha, Njwayo alisema utoro na mimba vimekuwa vikikithiri siku hadi siku katika wilaya hiyo kwa wanafunzi kuanzia darasa la pili.

Alisema kuna taarifa kutoka katika vyombo vya usalama kuwa wako wanafunzi wanaotoka nyumbani wakiaga wanaenda shuleni, lakini hawafiki na badala yake wanaishia kwenye vichaka kuvuta mihadarati na wengine kukaa maeneo ya ufukweni hadi jioni. "Wazazi tunatakiwa kubadilika, tuwafuatilie watoto wetu. Uhuru wanaopewa watoto ndio unaochangia wasithamini elimu na badala yake kufanya mambo wanayotaka na kusababisha tuendelee kushuka kwenye asilimia za ufaulu.

"Sasa ifike mwisho kila mtu awajibike kwa nafasi yake. Sitaendelea kuwavumilia wazazi wazembe wanaoshindwa kufuatilia maendeleo ya watoto wao," alisema.

Njwayo pia aliagiza kila shule kuweka kambi kwa wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya taifa kwa shule za msingi na sekondari miezi mitatu kabla ya mtihani.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Utete, Avit Mtema, alisema wanafunzi wanaoshindwa kufika shuleni wengi wao huishia kuzurura mitaani bila kazi.

Mtema alisema endapo kila mmoja atasimamia vizuri nafasi yake, utoro utakomeshwa na wanafunzi watakuwa wanafika shuleni na kuzingatia masomo hali ambayo itainua kiwango cha ufaulu kwa wilaya hiyo.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa moja ya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza, katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Rusoli, Musoma Vijijini, mkoani Mara jana, ambayo mwaka huu imepokea jumla ya wanafunzi 132. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# JPM ateua wenyeviti wa bodi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewateua wenyeviti watatu wa bodi za taasisi mbili za serikali na moja ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema Rais Magufuli amemteua Gabriel Malata kuwa Mwenyekiti na Mjumbe wa kuiwakilisha serikali katika Bodi ya kampuni ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania Ltd. Malata ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Pia taarifa hiyo ilibainisha kuwa Rais amemteua Prof. Martha Qorro kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kilichoko Dodoma. Prof. Qorro ni Profesa Mshiriki wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais amemteua Prof. Joseph Rwegasira Buchweshaija kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) iliyoko Arusha.

Taarifa hiyo ilimkariri Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi kuwa uteuzi wa viongozi hao ulianza juzi. Katika hatua nyingine, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchuka, amewateua makatibu tawala wapya wanane wa wilaya na kuwahamisha watatu vituo vya kazi.

Walioteuliwa na vituo vya kazi kwenye mabano ni Michael Semindu (Mbarali), Mikidadi Nchunguye (Kigoma), Lincoln Tamba (Mlele), Neema Nyalege (Kiteto) na Estomih Kyando (Iringa).

Taarifa ya uteuzi huo iliwataja wengine kuwa ni Hoffman Sanga (Mvomero), Amin Mrisho (Mwanga) na Nicodemus Shirima (Bariadi). Waliohamishwa vituo ni Veronica Kinyemi kutoka Bariadi kwenda Mkuranga, Delmina Tumaini kutoka Mwanga kwenda Kigamboni na Rahel Mhando kutoka Kigamboni kwenda Korogwe.

Wateule wapya, kwa mujibu wa taarifa hiyo, wanatakiwa kuripoti Februari 4, mwaka huu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukamilisha taratibu za uteuzi.

## Afariki dunia kwa kutumbukia kisimani

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKAZI wa kijiji cha Nkomolo, Nkasi mkoani Rukwa, Elisha Mgaya (32), amefariki dunia baada ya kuteleza na kutumbukia kwenye kisima cha maji wakati akijaribu kuvitoa vitoto vya paka wake vilivyotumbukia kwenye kisima hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alisema juzi kuwa tukio hilo lilitokea Januari 29, mwaka huu, majira ya saa 10 jioni karibu na nyumba aliyokuwa akiishi Mgaya na familia yake.

Alisema siku ya tukio hilo, watoto hao wa paka walitumbukia katika kisima cha maji kilichoko pembeni ya nyumba yake ambacho alikuwa akikitumia kwa ajili ya kupata maji ndipo akaamua avitoe kisimani.

Kamanda Maseji alisema akiwa anaendelea na harakati hizo kwa kutumia kamba na kopo, ghafla aliteleza na kutumbukia katika kisima hicho.

"Kwa kuwa alikuwa akifanya kazi hiyo peke yake, ilikuwa vigumu kupata msaada wa kuokolewa kitendo kilichosababisha kunywa maji mengi na kisha kuzidiwa na kufariki dunia," alisema.

Baada ya muda, alisema majirani walianza kumtafuta kutokana na kutoonekana kwa muda mrefu na hatimaye kukuta mwili wake ukielea ndani ya maji na kuuopoa kisha kuupeleka Kituo cha Afya cha Nkomono kwa uchunguzi kabla ya kukabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya maziko.

Kamanda huyo wa polisi alisema kutokana na tukio hilo, hakuna mtu yeyote anayeshikiliwa.

# Zungu atoa angalizo wafanyakazi wizara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, ameemtaka kila mtumishi katika ofisi hiyo kuwajibika ipasavyo mahali pa kazi na kuepuka kujihusisha na vitendo visivyokuwa vya kimaadili.

Zungu alitoa angalizo hilo jana jijini Dodoma, wakati akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo, akiwakumbusha kuwa serikali imedhamiria kwa dhati kuimarisha utendaji kazi ili kufanikisha dhana ya Tanzania ya Viwanda.

"Ninafahamu kwamba watumishi wana malalamiko yanayohusu kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu na upungufu wa watumishi katika idara na vitengo, malalamiko haya ni mtambuka katika wizara zote kwani yametokana na uhakiki wa vyeti vya elimu, zoezi lililoendeshwa na serikali kuanzia mwaka 2016.

"Ninawashauri muwe na subira wakati serikali ikiimarisha mifumo yake ya usimamizi wa rasilimali watu," alisema.

Waziri Zungu pia alibainisha kuwa baraza la wafanyakazi ni jukwaa muhimu mahali pa kazi kwa kuwa ni kiunganishi kati ya menejimenti na wafanyakazi, hivyo aliwataka kuendeleza ushirikiano ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya ofisi na taifa kwa ujumla.

"Watumishi wenzangu, hakikisheni mshahara mnaopewa mnautendea haki. Msitake kupata mshahara wa bure! Fanyeni kazi kwa bidii," Zungu aliagiza.

Aliongeza kuwa kuwapo kwa mabaraza ya wafanyakazi katika taasisi ni matakwa ya kisheria kwa madhumuni ya kuishauri serikali katika ngazi za idara na ofisi ili kuhakikisha majukumu yanatekelezwa ipasavyo, kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi.

Aliwakumbusha kuwa wajibu wa mabaraza hayo kama vyombo vya ushauri na usimamizi, ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao na kuzingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo chanya katika utendaji kazi.

Ajenda na madhumuni ya mkutano huu ni kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha nusu mwaka cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/20.



Rundo la magunia ya mkaa yakisubiri wateja nje ya soko la Urafiki maarufu 'Mahakama ya Ndizi', jijini Dar es Salaam wikiendi. Wananchi wanatakiwa kuelimishwa kuhusu matumizi ya teknolojia ya nishati mbadala ambayo ni rahisi na yenye uhakika ili kupunguza matumizi ya mkaa yanayosababisha ongezeko la matukio ya ukataji wa miti ovyo. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkemia ajivunia mtambo wa kisasa Kanda ya Ziwa

**Na Mary Geofrey,** MWANZA

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Kanda ya Ziwa, katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, imefanikiwa kununua mitambo ya kisasa ijulikanayo AAS na DR 5,000 inayowezesha uchunguzi wa sampuli za uchafuzi wa mazingira.

Pia imesema imenunua mtambo wa kisasa ujulikanao GC kwa ajili ya kuchunguza sumu mbalimbali kwenye sampuli zinazopelekwa katika maabara hiyo.

Hayo yalielezwa jana na Meneja wa GCLA Kanda ya Ziwa, Bonaventure Masambu, wakati akizungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika ziara ya kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

Ziara hiyo ina lengo la kuangazia mafanikio ya sekta ya afya katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano na malengo ya baadaye.

Alisema kuwapo kwa mitambo hiyo kumesaidia kuboresha huduma zinazotolewa na maabara hiyo na kusaidia kupunguza muda wa kuchunguza sampuli.

Alisema awali sampuli hizo zilikuwa zinapelekwa jijini Dar es Salaam kufanyiwa uchunguzi na baadaye majibu kurejeshwa ofisi za kanda. "Kwa sasa, maabara yetu ya kanda ina uwezo wa kufanya uchunguzi wa aina zote za sumu. Hii inatufanya tujisikie faraja zaidi kwa sababu lengo letu ni kuhudumia wananchi kwa ukaribu zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa mafanikio mengine wameongeza uchunguzi wa maabara kutoka sampuli 1,085 mwaka 2015 hadi sampuli 7,193 mwaka 2019.

Masambu aliendelea kuelezea mafanikio mengine ni kufanya ukaguzi wa maeneo yenye kemikali kutoka maeneo 151 mwaka 2015 hadi 213 mwaka 2019.

Alisema pia idadi ya vibali walivyotoa vya kuingiza na kutoa kemikali nchini kupitia mipaka ya Kanda ya Ziwa imeongezeka kutoka 1,350 hadi 2,246.

"Vibali tunavyotoa vimeongezeka kwa sababu kulikuwa na wadau wengi waliokuwa wakipitisha kemikali bila vibali, lakini baada ya kupewa elimu ya kufuata sheria na kuzuia kemikali hatarishi zilizokuwa zinazoingia nchini," alisema.

Masambu alitaja mafanikio mengine kuwa ni utoaji wa elimu kuhusu faida ya matumizi salama ya kemikali, watumiaji wa kemikali katika uchenjuaji ambao wameongezeka kutoka 183 mwaka 2015 hadi 592 mwaka 2019.

Alisema kuwapo kwa ongezeko hilo la wachenjuaji kwa kutumia kemikali, limewavutia wauzaji kuongezeka kutoka 15 mwaka 2015 hadi 92 mwaka 2019 na wasafirishaji walianza kutoa huduma ambao wapo 14.

# Watoto watano waungua moto kila siku Kahama

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Dk. George Masasi, amesema kuwa wastani wa watoto watatu hadi watano wilayani humo huungua moto au maji ya moto.

Dk. Msasi aliiambia Nipashe juzi hospitalini hapo kuwa watoto ndiyo wamekuwa waathirika wakubwa wa ajali za moto na maji yaliyochemka kutokana na kuwekwa sehemu ambayo si salama.

Alisema baadhi ya wazazi ni wazembe katika ulinzi wa watoto kutokana na kuweka jiko eneo hatari kwa watoto, chai au uji sehemu ambayo mtoto anaweza kupenyeza na kuungua.

"Kwa siku ni watoto watatu hadi watano wanaoletwa hospitalini hapa kutibiwa na kulazwa wakiwa na majeraha ya kuungua na moto au maji ya moto, ambayo wazazi walikuwa wakichemsha na jiko kuwekwa eneo la hatari bila kuangalia usalama wa watoto," alisema.

Dk. Masasi aliongeza kuwa huduma iliyokuwapo pindi wakifikishwa hospitalini hapo, ni kuongezwa damu haraka ili wasipoteza maisha kwa kuwa kitaalamu seli za mwili zinakuwa zimekwishaungua kutokana na moto na husababisha kupunguza kwa wingi wa damu mwilini.

Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Kahama, Abdulahamu Nuru, alisema wazazi wengi wanaona suala la kuungua kwa watoto ni kawaida, lakini wanatakiwa kutoa ulinzi kwa watoto kisheria.

"Baadhi ya wazazi wamekuwa wakiacha jukumu la kulea watoto kwa watoto wenzao, na wao kwenda kwenye shughuli za kilimo na utafutaji. Inakuwa rahisi huku nyumbani watoto kupatwa na ajali za moto," alisema.

Getrude Shija, mkazi wa Kata ya Nyihogo na Mhoja Selestine, mkazi wa Nyasubi, waliokuwa watoto wao wamelazwa hospitalini hapo kutokana na ajali za moto, walisema walikuwa wakichemsha maji ndipo watoto wao waliokuwa wakikimbizana wakaparamia jiko na kuungua.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Weledi wahitajika zaidi kuandaa ratiba Ligi Kuu*

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara unakaribia kumalizika na kuanza kwa raundi ya lala salama ya ligi hiyo, zipo klabu nyingine zina mechi mkononi maarufu ikijulikana kwa jina la viporo.

Suala la viporo limeonekana kuwa tatizo sugu katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa vigezo la baadhi ya timu kuwa na majukumu kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano ya kimataifa.

Michuano hiyo ya kimataifa imekuwa ikishirikisha timu za nchi zote, lakini kwa hapa nchini imeonekana kuwasumbua zaidi wahusika wanaopanga ratiba na kupelekea baadhi ya timu kuwa nyuma kwa idadi ya mechi ukilinganisha na klabu nyingine.

Msimu uliopita tulishuhudia waliokuwa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam kuwa na viporo vya mechi zaidi ya tano, jambo ambalo liliifanya timu hiyo baadaye kupangiwa mechi mfululizo.

Simba ilijikuta na jukumu la kucheza mechi kila baada ya siku moja, jambo ambalo ni kinyume na kanuni za ligi hiyo, lakini haikuwa na uwezo wa kupinga na badala yake ilicheza viporo hivyo walivyokuwa navyo.

Lakini kwa kuangalia mapungufu yaliyojitokeza msimu uliopita, Nipashe na wadau wengine wa soka nchini walidhani suala hili litakuwa fundisho na kupata ufumbuzi kwa msimu huu, hali imekuwa tofauti.

Msimu uliopita, Simba ilifika hadi hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini msimu huu, Yanga ambayo iliishia hatua ya mtoano imeonekana kuwa na viporo vingi mapema.

Viporo hivi si tu vinaonekana kutengeneza mazingira ya kupanga matokeo, lakini vinapunguza ushindani baina ya timu kwa sababu tayari picha ya bingwa huanza kuonekana kwa timu zinazopambana kuwania taji hilo.

Mbali na mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Simba, pia kuna vita nyingine ya kujiepusha na janga la kushuka daraja ambalo msimu huu itakuwa kubwa zaidi kutoka na idadi ya timu zinazotakiwa kuteremka kuongezeka.

Kujifunza au kugeza kwa nchi zilizoendelea si dhambi, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB), msisite kwenda kutafuta msaada wa upangaji wa ratiba kwa vyama vya soka vilivyoendelea.

Kufanya hivi kutasaidia kumaliza malalamiko ambayo yanaendelea kutolewa na klabu pamoja na wadau wanaofuatilia ligi hiyo na vile vile itasaidia kuongeza thamani ya ligi yetu tunayoitegemea kuzalisha wachezaji wengi wanaoitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Nipashe tunasema bado hatujachelewa, wahusika wanaweza kuwaita wenye uzoefu wa kupanga ratiba na kumaliza malalamiko ambayo yanaendelea kuhusiana na ratiba hiyo.

Ushauri huu ni maalumu kwa sababu bila ya kushirikisha wadau, mambo yanaweza kuwa mabaya zaidi huko mbele kwa sababu kabla Ligi Kuu msimu wa 2019/20 haujamalizika, kikosi cha Stars kitatakiwa kuingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) ambazo zitachezwa kuanzia Aprili 4 hadi 25, mwaka huu huko nchini Cameroon.

Upangaji huo mpya wa ratiba kama utafanyika, ni muhimu kuzingatia muda wa mechi moja hadi nyingine kwa maslahi ya afya za wachezaji ambao taifa linawahitaji kwenda kupeperusha vizuri bendera ya nchi katika fainali hizo ambazo Tanzania tunashiriki kwa mara ya pili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Simba, Yanga zinavyohasiriana!*

Na Barnabas Maro

**"ADUI** wa mtu ni mtu," chambilecho wahenga, yaani babu zetu. Maana yake binadamu huhasiriwa (fanyiwa matendo ya kumdhuru au kumwumiza kimwili na kiakili) na binadamu mwenzake.

Hii ni methali ya kutukumbusha kuwa aghalabu (hali ya kutokea jambo mara nyingi; ghalib) matatizo tuyapatayo husababishwa na watu tunaoishi nao kila siku.

'Mtani' ni mtu anayemfanyia mwingine dhihaka. Mtu aghalabu wa kabila tofauti au rafiki mkubwa ambaye ameruhusiwa kumdhihaki mwingine kwa mujibu wa mila zao bila anayetaniwa kukasirika.

Husemwa eti/ati (neno la kuonyesha shaka ya jambo au kutokuwapo uwezekano) Simba na Yanga ni 'watani wa jadi!' Nielewavyo, maana ya 'utani' ni maneno au vitendo vya dhihaka; masihara kwa mwingine au wengine.

Sioni huo uitwao 'utani wa jadi' wa Simba na Yanga ila lililopo ni chuki, wivu na kuombeana mabaya! Kama huo ndio 'utani wa jadi,' sikubaliani nao abadan (katu)!

"Afiriti hafichiki." Afiriti ni mtu mwovu au mwenye matendo maovu. Maana yake mtu m-baya hafichiki.

Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa uovu wa matendo mabaya hayawezi kufichika; lazima kuna siku yatajitokeza. Yaweza kutumiwa kumgutua (kumtanabahisha) mtu mwovu aache uovu wake.

Kwa nini timu huambiwa na wachawi au waganga zibadili njia zitakazopita kwenda na kuingia uwanjani na mchezaji atakayetangulia kushuka kwenye gari na atakalofanya baada ya kushuka!?

Huo ndio 'utani wa jadi?' Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.)

Hakika timu hizo zafaa kufanyiwa ifaki yaani hali ya kuwarejesha watu katika imani yao ya awali.

'Ushirikina' ni upotovu wa hisi (fahamu au tambua kitu kwa kutumia milango ya fahamu ya kugusa, kuonja, kunusa, kuona au kusikia) za dini na wa matendo yanayotakiwa na hisi hizo.

Waweza hata kuathiri uchaji tunaompa Mungu wa kweli. Mfano, mtu anapotoa umuhimu ulio wa kichawi, kwa namna fulani, kwa matendo fulani ambayo kwa yenyewe ni halali au lazima.

Namna zote za kupiga bao lazima kuzikataa; kumwendea shetani au mapepo, kuwaendea wafu au matendo yoyote potofu yanayofikiriwa "kufunua" wakati ujao.

Kuuliza kwa kuagua kwa njia ya nyota, unajimu, usomaji kiganja, tafsiri ya fali (ndege m-baya), matukio ya nguvu inayodaiwa kuna mambo yasiyoonekana na wengine, kukimbilia vijumbe vyote huficha hamu ya nguvu juu ya nyakati, historia na mwishowe watu wengine na pia kutaka kujipatanisha na nguvu zilizofichika.

Yote haya yanapingana na heshima, hadhi na uchaji wa mapendo tunayowiwa na Mungu peke yake.

"Kwa hiyo ujue, leo hivi, ukaweke moyoni mwako, ya kuwa Bwana ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini; hapana mwingine."

'Umbeya' pia 'umbea' ni tabia ya kutoa habari bila ya kutumwa au kuulizwa; udaku, udakuzi. Tabia ya kufuatilia au kusikiliza habari za watu wengine bila kutumwa; ubemba.

Vilabu vya Simba na Yanga vina wasemaji wao. Hao ni watu maalumu walioajiriwa kutangaza mambo ya vilabu hivyo baada ya kujadiliwa kwa kina na viongozi. Baadhi ya mambo hayo, kuna yanayotakiwa kuwekwa wazi ili wanachama wajue. Kwa utaratibu huo, pia kuna baadhi ya mambo yasiyotakiwa kuwekwa hadharani.

Hata hivyo kuna viongozi wambeya, wasiokuwa na vifua vya kuficha siri. Mfano ni wakati wa usajili wa wachezaji wapya. Usajili wa timu za Simba na Yanga hauna siri na wanaotoa habari hizo ni baadhi ya viongozi wambeya wasiotaka majina yao kutajwa magazetini!

Watu hao pia huwaeleza wanachama na mashabiki wao. Hivyo mambo huwa hadharani kwa wanachama na mashabiki kuwaringia wenzao wa upande wa pili waitwao 'watani wa jadi!'

Siri inapotoka nje, huwa na hekaheka ya upande mwingine kuingilia kati na kuchafua mambo katika kile kisemwacho: "Tupate sisi, vinginevyo tukose wote." Huo ndio 'utani wa jadi' wa Simba na Yanga. Salala! (tamko linalodhihirisha hisia ya mshangao.)

Mwalimu wa kandanda ambaye kwa jina lingine aitwa kocha, ndiye anayejua umahiri na udhaifu wa wachezaji wake tangu wanapokuwa mazoezini. Kwa hiyo anapopanga wachezaji watakaoanza ana sababu zake.

Viongozi hawatakiwi kumwingilia kocha anapopanga wachezaji kama ilivyozoeleka kwa vilabu vya Simba na Yanga. Kama wao wanajua, kwa nini wanaajiri makocha kwa fedha nyingi badala ya mmoja wao kujitolea kuwa kocha?

Methali ifuatayo yawafaa viongozi wanaojitia kimbelembele katika mambo wasiyojua: "Usijigeuze chano watu wakakufulia."

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Dampo la kisasa kujengwa Dar

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amesema serikali inatarajia kujenga dampo la kisasa katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kuhimili taka zote zinazozalishwa mkoani humo.

Zungu aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kujenga madampo mengine katika wilaya zote za mkoa huo kwa kuwa hivi sasa kuna dampo moja la Pugu Kinyamwezi.

Waziri huyo alibainisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 75 kimetolewa na wafadhili kwa ajili ya kazi hiyo ambayo itakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami katika eneo la dampo ili kurahisha usafirishaji wa taka na Halmashauri ya Jiji hilo tayari imetenga fedha.

"Kasi ya taka zinazozalishwa Dar es Salaam ni kubwa na jiji linakua kwa asilimia kubwa sana na kwa miaka miwili ijayo kasi ya 'population' (idadi ya watu) itafika milioni nane hadi tisa na dampo ni moja na juzi mimi nilitembelea dampo hilo, hali yake ni mbaya, lazima tukiri hali ni mbaya, miundombinu ni mibaya, hatua zimeshachukuliwa," alisema.

Awali, akijibu swali la msingi la Mdee kuhusu mkakati wa serikali kukabiliana na tatizo la uchimbaji mchanga na uchafuzi uliokithiri jijini humo, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, alikiri uchimbaji huo huleta athari ikiwa ni pamoja na mmomonyoko wa kingo za mito, uharibifu wa maji, miundombinu na mwingiliano wa maji ya bahari katika nchi kavu.

Alitaja athari zingine kuwa ni kubadilika kwa mkondo wa mto kutoka uelekeo wa asili, kuharibika kwa uimara wa mto, uharibifu wa mimea ya asili ambayo husaidia kupungu mmomonyoko na uharibifu wa mazalia ya viumbe hasa wakati kina cha maji kinapoongezeka.

Alisema serikali inaandaa mkakati wa muda mrefu unaotokana na mapendekezo ya kamati maalum ya wadau iliyoundwa na ofisi hiyo kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuwa na uchimbaji endelevu wa mchanga na usiokiuka sheria za nchi.



Wafanyakazi wa kampuni ya Nyanza Road, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Kitunda hadi Kivule kwa kiwango cha lami, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC atangazia kiama watumishi watoro

**Na Marco Maduhu,**
KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ametangaza kuanza kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani hapa kutokana na kuchelewa na utoro kazini.

Telack alibainisha hayo juzi akiwa kwenye ziara ya kikazi kwenye halmashauri hiyo kukagua utendaji wa kazi na miundombinu ya shule. Katika ziara hiyo alikumbana na changamoto ya uchelewaji na utoro kwa watumishi wa umma. Alisema uchelewaji na utoro kwa watumishi wa umma kwenye halmashauri hiyo vinatokana na baadhi yao kushindwa kuhamia kwenye makao makuu ya halmashauri na kubaki kuishi mjini Kahama, hivyo kuagiza watumishi wote wahamie kwenye maeneo yao ya kazi, kabla ya kuanza kuwachukulia hatua.

"Hapa ninapokagua daftari la mahudhurio la watumishi kwenye halmashauri hii, nimebaini kuna tatizo la uchelewaji na utoro kwa watumishi. Tatizo hili linatokana na kuishi nje na maeneo yenu ya kazi, ambapo mnaishi Kahama mjini. "Naagiza watumishi wote ambao hawajahamia hapa, nipatiwe majina yao na ninatoa siku chache wawe wamehamia hapa. Tofauti na hapo nitaanza kuwachukulia hatua kali za kinidhamu," alisema Telack.

Sambamba na hilo, aliagiza wakuu wote wa shule kudhibiti utoro kwa wanafunzi shuleni pamoja na kufundisha kwa bidii ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi ikiwa kipaumbele cha mkoa huo ni elimu kwanza.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, aliendelea kuwasihi watumishi wa umma kufuata sheria na kanuni za kazi na kila mmoja asimame kwenye nafasi yake ya utekelezaji wa majukumu badala ya kuanza kusukumana.

# Mawakili kesi ya vigogo Acacia wageukia mazungumzo Barrick

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili rais wa zamani wa migodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu, Deogratius Mwanyika na wenzake, umeiomba mahakama kuuamuru upande wa Jamhuri kufuatilia mazungumzo kati ya serikali na Kampuni ya Barrick kuhusu kuondoa kesi zinazowakabili wateja wao.

Madai hayo yalitolewa jana na Wakili wa Utetezi, Lwekama Rwekiza, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Rwekiza alidai kuwa kuna mazungumzo kati ya serikali na Kampuni ya Barrick, ambayo ndiyo inasimamia kampuni ambazo washtakiwa ni waajiriwa.

Awali, Wakili wa Serikali, Gloria Mwenda, alidai mahakamani hapo kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na akaiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo.

Rwekiza alidai kuwa anakubaliana na upande wa Jamhuri na kwamba amewasilisha hoja yake na wakili anayeendesha kesi hiyo angekuwapo mahakamani hapo, angetoa majibu ya wapi walipofikia.

Alidai kuwa anaomba tarehe ijayo Jamhuri iwasilishe majibu kamili ya hoja yao.

Alidai kuwa kesi hiyo inahusiana na makubaliano yaliyotiwa saini hivi karibuni kati ya serikali na Kampuni ya Barrick kuashiria kumalizika kwa mgogoro uliokuwapo awali. "Mheshimiwa Hakimu, kesi hii ina uhusiano na makubaliano yaliyotiwa saini kati ya serikali na Kampuni ya Barrick na vyombo vya habari vimeripoti kumalizika kwa mgogoro baina ya serikali na kampuni hizi kwa kuanzishwa Kampuni ya Twiga ambayo serikali ni mbia, hivyo naiomba mahakama yako ielekeze Upande wa Mashtaka kufuatilia na kuona namna ya kufuta shauri hili." Wakili wa Utetezi alidai.

Upande wa mashtaka ulikubaliana na hoja za utetezi na kuahidi kufuatilia suala hilo na kuwaletea majibu.

Mwanyika na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 39, likiwamo la kutakatisha fedha na kukwepa kodi zaidi ya Dola za Marekani milioni 112.

Mbali na Mwanyika, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Bulyanhulu, Alex Lugendo, Mkurugenzi Mtendaji wa Pangea, North Mara na Bulyanhulu, Assa Mwaipopo, Kampuni ya Mgodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, 2018.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya kula njama, saba ya kughushi, 17 ya utakatishaji wa fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), kuongoza uhalifu wa kupangwa, manane ya kukwepa kodi na moja la kutoa rushwa.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Aprili 11, 2008 na Juni 30, 2007 katika sehemu tofauti za Jiji la Dar es Salaam, Kahama mkoani Shinyanga, Tarime mkoani Mara, Biharamulo mkoani Kagera, maeneo ambayo yapo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# Ubunge wa Zitto sasa njia panda

INATOKA UK. 2

ukwaji gani anaouona kuhusiana na jambo hilo katika taratibu za kibunge.

Aliposimama kwa mara nyingine, Dk. Mollel alisema: "Sisi tuliapa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tulipoapa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeapa kuilinda na kuiheshimu.

"Na hapa hatuhitaji kuingilia uhuru wa wabunge husika na hatuhitaji kuingilia uhuru wa mtu binafsi wa kutoa mawazo yake, lakini kikubwa hapa tunachoangalia wote, hapa tuliapa namba moja kwa ajili ya kulinda maslahi ya Tanzania.

"Kwa hiyo wakati unataka kutoa mawazo yako ambayo una uhuru wa kuyatoa wakati hutafakari usalama wa taifa lako kiuchumi na tafakari katiba ambayo umeapa kuilinda."

Kutokana na hoja hiyo ya Dk. Mollel, Spika Ndugai alifafanua jambo hilo akisema anavyopima hoja hiyo ni nzito maana ni hoja inayohusu usaliti kwa taifa.

**MJADALA MZITO**

Baada ya hoja hiyo uliibuka mjadala miongozi mwa wabunge huku upande mmoja ukijaribu kupinga na mwingine kuunga mkono suala hilo lijadiliwe.

Mbunge wa Nchinga (CUF), Hamidu Bobali, dharura alisema hajapata bahati ya kuona nakala ya barua hiyo, lakini anavyojua pamoja na kuwa Zitto ni Mbunge, pia ni Kiongozi Mkuu wa chama cha siasa na inawezekana kwenye nakala ya barua hiyo, ama ametia saini kama Kiongozi Mkuu wa Chama au Mbunge.

Kwa upande wake, Mbunge wa Ifakara (Chadema), Peter Lijualikali alisema hoja ya Dk. Mollel ya kusema kwamba Benki ya Dunia imeinyima mkopo Tanzania kwa sababu ya Zitto, serikali ilipaswa ndiyo iwaambie.

Naye Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde, alishauri kabla Bunge halijaingia katika mjadala, ilikuwa vizuri serikali itoe kauli kwa sababu wanaona jambo hilo kwenye mitandao ya kijamii ya instagram, whatsaap na twitter kwamba pesa zimezuiwa.

Mbunge wa kuteuliwa, Abdallah Bulembo (CCM) akichangia hoja hiyo, alisema mwanasiasa huyo hatakiwi kurudi Bungeni.

Mbunge wa Ileje (CCM), Janeth Mbene aliunga mkono maelezo ya Bulembo kwa kusema: "Kitu kinachonigusa ni maslahi ya taifa. Mtu anapotamka jambo lolote lile hasa anapokuwa kiongozi, lazima ajiulize hii inasaidia vipi taifa langu.

"Kitendo alichokifanya mwenzetu Zitto ni usaliti, lakini vile vile wazungu wanasema hakufikiria vizuri juu ya hili jambo. Kutofautiana mitazamo kuhusu wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni, haimpi uhalali yeye wa kwenda kufanya usaliti alioenda kuufanya."

Mbunge wa Korogwe Mjini (CCM), Mary Chatanda, alisema Zitto ni msaliti maana amewasaliti wabunge kwa kutumia nembo ya Bunge kinyume kabisa na sheria.

**APELEKWA KWA AG**

Kutokana na michango hiyo ya wabunge, Spika Ndugai alisema anapomsikia mtu anasema Benki ya Dunia wasitoe fedha, serikali ikapata ili kuboresha elimu, anashindwa kuelewa ni kwa nini, tatizo ni nini kwa sababu hata mtu awe mpinzani vipi, kuna mahali ambapo kidogo anasita.

"Lakini sasa niseme tu kwamba katika jambo hili kuna dalili za ujinai fulani kwa hiyo tumwombe AG (Mwanasheria Mkuu wa Serikali) hilo tulitupe huko. Zaidi mwangalie mkiona kuna ujinai katika jambo hili basi mchukue hatua.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adeladeus Kilangi, alisema ofisi yake imeyapokea maelekezo hayo na itayafanyia kazi.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na takataka zilizotelekezwa bila ya kuondolewa kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, jana, kitendo ambacho ni uchafuzi wa mazingira na hatari na zinaweza kusababisha magonjwa ya milipuko kama vile kipundupindu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Saa tano dakika 13 za Lugola Takukuru

INATOKA UK. 2

Mambo ya Ndani ya Nchi wa Sh. trilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Jeshi la Zimamoto.

Rais Magufuli alisema viongozi wa wizara hiyo walitia saini makubaliano ya zabuni ya kununua vifaa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji vyenye thamani ya Euro milioni 408.5 (sawa na zaidi ya Sh. trilioni moja) kutoka kampuni moja ya nje bila kufuata sheria.

"Kulikuwa na mkataba wa ovyo unaotengenezwa Wizara ya Mambo ya Ndani wenye thamani ya Euro milioni 408. Umetayarishwa na kusainiwa na Kamishna Jenerali wa Zimamoto, haujapangwa kwenye bajeti, haujapitishwa na Bunge.

"Wakati wa vikao na kampuni moja ya Romania, wahusika wa Tanzania walipokuwa wanakwenda kwenye majadiliano wanalipwa 'seating allowance' (posho ya vikao) ya Dola 800 (Sh. 1,832,170) na hata tiketi za ndege walilipiwa.

"YanayoAkwenda kununuliwa kule kwenye mkataba ni ya ovyo, ni ya ajabu, ukitaka kuvunja, yale ambayo yameshaanza kutekelezwa lazima yaendelee kutekelezwa,"

Rais Magufuli alisema na kuagiza wote waliohusika wahojiwe na hatua zichukuliwe.

## Mbunge ataka sheria ya mikopo elimu ifumuliwe

INATOKA UK. 2

Dar es Salaam baada ya kutishia kuandamana ili wanafunzi wapewe fedha za mikopo.

Katika swali la msingi, Lyimo alisema marejesho ya mikopo ya elimu ya juu yameendelea kukumbwa na tatizo kubwa hasa baada ya ongezeko la asilimia sita kama tozo ya kutunza thamani ya fedha na hivyo kusababisha wanufaika wa mikopo kushindwa kumaliza kurejesha mikopo hiyo.

Akimjibu mbunge huyo, Ole Nasha alisema serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) hutoza asilimia sita kwenye salio la deni la mnufaika wa mkopo kama tozo ya kutunza thamani.

Alieleza lengo la tozo hiyo ni kulinda thamani ya fedha wanazokopeshwa wanufaika wa mikopo ili kuwa na mfuko endelevu utakaoendelea kutoa mikopo kwa wahitaji wengine bila kulazimika kuongeza fedha zaidi kutokana na upotevu wa thamani ya fedha.

"Kumbukumbu zinaonyesha kuwa wanufaika wanaoanza kurejesha mikopo yao kwa wakati, humaliza kati ya miaka minne hadi 10 kulingana na kiwango cha mshahara," alisema.

Agosti 9 na 13, mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti iliyoibua kile kilichodaiwa uonevu katika urejeshaji wa mikopo hiyo. Wanufaika wengi wakilalamikia deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka na asilimia moja inayotozwa kwa ajili ya uendeshaji wa bodi.



Mtaalamu wa sayansi ya wadudu waharibifu wa mimea wa Taasisi ya Utafiti na Uendelezaji wa Mboga kwa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (WVC), Dk. Simon Boniface (kushoto), akifafanua jambo kwa Mwakilishi wa Shirika la Chakula Duniani (FAO) Tanzania, Fred Kafeero (katikati), aliyetembelea taasisi hiyo, jijini Arusha juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Gabriel Rugalema. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Halmashauri yamaliza mgogoro wa muda mrefu

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, limetatua mgogoro wa muda mrefu kati ya mwekezaji Sailepu Mollel na wananchi wa Kijiji cha Kitwai.

Mgogoro huo ulihusisha mwekezaji huyo ambaye alipeleka mifugo yake kijijini hapo mwaka 2017 na kuandika barua ya kuwa mwanakijiji mwaka uliofuata, hatua iliyosababisha baadhi ya wananchi kumkubali na wengine kumkataa wakimhusisha na masuala ya kisiasa.

Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Baraza la Madiwani, Sendeu Laizer, alisema juzi kuwa waliwahoji wajumbe 18 wa serikali ya kijiji ambapo kati yao 11 walimkubali na saba walimkataa.

Sendeu alisema wengine walisema Mollel amemaliza ujenzi wa madarasa matatu ya shule ya msingi, zahanati na amechangia fedha katika baadhi ya kwaya.

"Kuna mjumbe alieleza kuwa baadhi ya watu walidai kwamba kuna maneno yalisambazwa na wapambe waliokuwa wanasema Mollel ana mkono mrefu kuliko wa Mungu," alisema.

Diwani wa Naisinyai, Kilemp Ole Kinoka, alisema wananchi wa kijiji hicho wanapaswa kutambua kuwa kila Mtanzania anaweza kuishi popote ili mradi havunji sheria.

"Yule ni mfugaji kama walivyo wanakijiji hicho. Tusikatae wageni hata hapa Orkesumet kuna kina Ngunda wamekuja muda mrefu. Tupo nao na tunakunywa soda pale kwao," alisema Ole Kinoka.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jackson Sipitieck, alisema ameunda timu ya madiwani ili wakafanye mkutano wa wananchi kwenye kijiji hicho ukimuhusisha Mollel.

Sipitieck alisema baadhi ya madiwani hao ni Ezekiel Lesenga (Mardad), Ole Kinoka, Alamayan Ranga na Laizer. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Silvanus Tairo, aliwapongeza madiwani hao kwa uamuzi huo kwa kuwa Kijiji cha Kitwai kiko nyuma kimaendeleo. Tairo alisema mdau huyo amekuwa akichangia maendeleo kwenye kijiji hasa katika afya na elimu.

# RC Gambo ammwagia sifu Simbachawene

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amempongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, kwa askari wake kuanza vizuri mwaka kwa kuwaua watu watano waliotuhumiwa kwa ujambazi mkoani Arusha.

Alitoa pongezi hizo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na kuuawa watu hao wanaodaiwa walikuwa wakienda Simanjiro mkoani Manyara kufanya uhalifu.

"Hii ni dalili nzuri kwa Waziri Simbachawene. Yaani hata hajakaa mwezi tayari vijana wake wameonyesha wako imara katika ulinzi wa nchi na wananchi pamoja na mali zao," alisema.

Gambo alisema baada ya kusikia tukio hilo, alifurahi kwa kuwa amehakikishiwa mkoa huo wa utalii uko salama. Pia alisema Arusha ni mkoa wa utalii na unachangia asilimia 17 ya pato la taifa katika kutokana na mapato ya utalii.

Aliwataka askari hao kuongeza juhudi zaidi ili kukomesha matukio ya uhalifu kwa ajili ya kuwezesha watalii na wananchi wa mkoa huo kutembea kwa amani.

Watuhimiwa hao wa ujambazi waliuawa Januari 29, mwaka huu, majira ya saa 3:45 katika eneo la Mateves kwenye barabara ya Afrika Mashariki (Baypass) wakiwa kwenye pikipiki tatu.

# Msajili afungia machinjio nyama

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MSAJILI wa Bodi ya Nyama Tanzania, Imani Sichalwe, ameyafungia kutoa huduma baadhi ya machinjio kwa kukiuka masharti na taratibu za machinjio katika wilaya ya Arumeru na jijini Arusha.

Sichalwe alisema juzi kuwa amechukua hatua hiyo kwa mujibu wa sheria ili kuepusha madhara ya kiafya yanayoweza kuwapata

walaji kutokana na machinjio kukiuka masharti ya bodi hiyo.

Alisema machinjio yaliyofungiwa yamekuwa yakiweka ng'ombe chini wakati wa kuchinja na kuuza nyama katika makaratasi yaliyotandazwa chini na kucharanga nyama chini.

"Hawa wote wenye machinjio haya wanaweza kuona kuwa ni jambo la kawaida lakini kwetu bodi ni kosa kubwa kukiuka masharti maana kuweka nyama katika mazingira hayo, inaweza kupata wadudu kwa urahisi kutoka ardhini na kuumiza walaji. Sasa katika hili hatuna utani nalo kwa kweli," alisema Sichalwe.

Alitaja baadhi ya machinjio yaliyokutwa na kasoro na kufungiwa kuwa ni Samunge, Masai wilayani Arumeru na Tengeru jijini Arusha.

"Mfano hawa Tengeru tumewakuta na mitaro ya kupitishia maji machafu na damu inachafua sana mitaro hiyo. Pia wafanyakazi hawana sare ambazo ni mabuti na koti jeupe na usafi wa bucha haukuwa wa kuridhisha," alisema.

Sichalwe aliongeza kuwa atafanya ziara ya kushtukiza katika eneo la Kwa Murombo kukagua usafi na bucha ambazo hazipaswi kuwa mjini ambazo

yanachinjia wanyama kwenye makaro na si vifaa vya kisasa na vyenye usalama yatafungiwa pia.

"Wanaofikiri hizi ni nguvu za soda wapuuze maana kumekuwa na mazoea ya machinjio kufungiwa na wakiona kimnya wanaendelea. Ifike mahali sasa

tupeleke wanyama kwenye machinjio za kisasa na zinazokidhi vigezo vya usalama," alisema.

Alitoa onyo kwa machinjio yaliyofungiwa kutofungua bila ruksa ya bodi na wakifanya hivyo watachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.





# Kiwanda kusaidia jamii kiafya

**Na Daniel Sabuni,** MOSHI

KIWANDA cha kuzalisha sukari cha Kilimanjaro, Tanganyika Planting Co Ltd (TPC) kilichopo mjini Moshi mkoani Kilimanjaro kwa kushirikiana na Taasisi ya FEMI ya Uholanzi, wamejipanga kuzisaidia jamii inayozunguka kiwanda hicho kielimu, afya na miradi ya mingine.

Ofisa Mtendaji Mkuu Utawala wa TPC Limited, Jaffary Ally, alisema juzi kuwa kiwanda hicho kitatekekeza miradi endelevu ya kuisaidia jamii na tayari wameanzisha shirika lisilo la kiserikali la FTK Kilimanjaro.

Alisema FTK kila mwaka hutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mwaka huu wa fedha imetenga kiasi cha Sh. bilioni 1.4 na mwaka 2017/18 ilitenga Sh. bilioni 1.7.

"Fedha hizo zimetumika na zinaendelea kutumika kwenye ujenzi wa zahanati katika maneo ya vijiji vya Kirungu, Mserekia na nyumba za walimu, maabara, vyoo, madarasa, madawati na chakula kwa wanafunzi," alisema.

Ally alisema watoto wanaotoka katika kaya maskini, hupewa ufadhili kimasomo katika shule za sekondari hadi vyuo vikuu, taasisi hiyo ikitenga Sh. milioni 450 kwa ajili ya elimu pekee.

Alisema FTK wameweza kukarabati miundombinu kama madaraja na madarasa katika vijiji mbalimbali na zahanati katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka TPC.

"Mambo ya msingi tunayoyafanya kupitia FTK ni elimu, afya kwa vijiji, miradi mikubwa ya vijiji na miundombinu tunahakikisha ujirani mwema unatekelezwa kwa vitendo kwelikweli," alitamba.

Alisema TPC imewajengea watoto wa wafanyakazi shule nne za awali, shule za msingi tano na mbili sekondari na kuhudumia usafiri, miundombinu, madaftari, chakula na sare za shule.

# Ofisa Ardhi kortini tuhuma za rushwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro, imemfikisha mahakamani Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Hai, Wilbert Mayila, kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni moja. Kesi hiyo ya rushwa namba CC. 38 ya mwaka 2020 ilifunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Hai mbele ya Hakimu Mfawidhi Devota Msofe huku Takukuru ikiwakilishwa na Mwendesha Mashtaka, Suzan Kimaro.

Mwendesha Mashtaka Kimaro alidai Mayila anashtakiwa kwa makosa ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni moja kutoka kwa Spous Mushi kwa maelezo kwamba angemsaidia kupata hati ya kumiliki eneo lililoko mji mdogo wa Bomang'ombe.

Alidai Mayila alitoa madai hayo kwa Mushi na kujipatia fedha hizo kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007, huku akifahamu kwamba eneo hilo ni mali ya Shirika la Umeme (Tanesco).

Mshtakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na yuko nje kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana yaliyomtaka kuwa na mdhamini mmoja atakayetia saini bondi ya Sh. milioni mbili, na kesi hiyo itatajwa tena mahakamani hapo Machi 16, mwaka huu.




Mratibu wa mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja ya kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani Kilimanjaro, Veronika Ullomi (aliyesimama), akijadili jambo na wanaharakati wa Wilaya ya Mwanga juzi, kuhusu matukio ya ubakaji watoto. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wanaowatia mimba wanafunzi wamulikwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI wilayani Siha mkoani Kilimanjaro imesema haitawafumbia macho wanaume wanaosababisha wanafunzi kukatisha masomo kutokana na kuwatia mimba.

Mbali na mimba kwa watoto wawapo shuleni, serikali pia imesema itawafikisha kwenye mkono wa sheria wazazi wote watakaofanya makubaliano au mazungunzo baada ya mtoto kupewa mimba.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano maalum uliondaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organition (KWIECO) kwa lengo la kumlinda mtoto wa kike, Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, alisema mimba za shuleni hazikubaliki.

"Natoa rai kwa wazazi na walezi kuongeza umakini katika kumlinda mtoto wa kike ikiwa ni pamoja na kuwalinda dhidi ya ukatili wa kijinsia na ikibainika hatutalifumbia macho suala hilo na hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wahusika," alionya.

"Wazazi mna tabia ya kuombana msamaha wakati mtoto amefanyiwa ukatili au kufanya mazungunzo na baada ya kupewa kitu kidogo, mnakataa kutoa ushahidi mahakamani na kesi inakosa nguvu.

"Sasa, hatutawafumbia macho na hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwaburuza mahakamani wazazi wa mtoto aliyefanyiwa ukatili."

Elizabert Minde, Mkurungenzi (KWIECO), alisema lengo la kukutana na wanafunzi hao ni kujenga uelewa kwa lengo kutokomeza ukatili katika jamii hasa kwa watoto wa kike.

Minde alisema watoto wengi wamekuwa wakifanyiwa ukatili lakini ni waoga kutoa taarifa mara wanapofanyiwa ukatili, jambo ambalo limeanza kufanyiwa kazi kwa kutoa elime kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

"Serikali inatoa misaada mingi kuchangia elimu ili watoto wetu waweze kusoma, lakini sisi tumeona tuiunge mkono serikali katika kuendeleza elimu kwa kuwapa mbinu za kujilinda dhidi ya ukatili wa kijinsia ili waweze kumaliza elimu yao kwa usalama," alisema.

"Baadhi ya wazazi tumekuwa chanzo cha watoto wetu kupata mimba na wengine kuwa watoro shuleni, tunawapa uhuru usiokuwa na mipaka hali ambayo inawafanya wasiudhurie masomo, tuwafuatilie hatua kwa hatua ili kufikia lengo."



## HABARI DODOMA




Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakimsikiliza Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Msekeni Mkufya (hayupo pichani), kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika jijini humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kichere awawashia moto watumishi wa ofisi yake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATUMISHI katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT), wametakiwa kuwa mfano ili kupata uhalali wa kimaadili na kimamlaka katika kusimamia taasisi zingine.

Hayo yalisema jana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, katika ufunguzi wa mkutano wa kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa ofisi hiyo jijini hapa.

Alisema hakuna uvumilivu na masuala ya kutokuzingatia maadili kwa watumishi wa ofisi ya CAG.

"Ikitokea kuna tuhuma juu ya mtumishi yeyote, hakika taratibu za kisheria zitafuatwa na ikithibitishwa ni kweli maadili hayakufuatwa, mtumishi huyo hataendelea kuwa sehemu ya ofisi hii," alisema Kichere.

Alisema katika kuhakikisha wanasimamia vyema maadili ndani ya ofisi wamechukua hatua mbalimbali kwa watumishi wachache ambao wamekuwa na tuhuma za utovu wa maadili.

"Tumekubaliana kwamba kwa pamoja tutasimamia maadili ndani ya ofisi hii na yeyote ambaye atakiuka maadili na kuichafua ofisi hii, kwa pamoja tutamtosa ili ofisi ipone.

Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwaomba na kuwasihi wakaguzi wetu nao kuzingatia maadili kwenye ukaguzi. Kumekuwa na tuhuma mbalimbali zinazohusu watumishi wetu wachache ambao wengine wameshachukuliwa hatua, lakini tuhuma hizi pia inaonekana kuna wahusika toka upande wa wakaguliwa ambao wanashirikiana na watumishi wetu katika kukiuka maadili ya utumishi wa umma na ukaguzi. Ni vyema pande zote tukazingatia maadili ya utumishi wa umma," alisema Kichere.

Aidha, alisema katika kuhakikisha wakaguliwa na wakaguzi wanaelewa majukumu yao na nini cha kufanya wakati wa ukaguzi na kwamba Desemba mwaka jana, alitoa waraka kwenda kwa maofisa masuhuli wote ili wauzingatie na kuwasihi kuzingatia yaliyomo kwenye waraka.

Kichere alisema ili kubobea na kuwa na utaalamu wa kutosha katika maeneo haya mapya katika ukaguzi, ofisi inahitaji watumishi kupatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi kulingana na mahitaji ya ofisi.

"Pamoja na mafunzo, ofisi inahitaji vitendea kazi vya kisasa ili kuongeza ufanisi wa ukaguzi katika maeneo yote yaliyotajwa hususani ukaguzi wa kina na wa thamani," alisema. Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga, aliwasihi wafanyakazi kuhakikisha wanazingatia kikamilifu na kwa makini kwenye masuala yote yatakayojadiliwa katika mkutano huo.

Maganga alisema hayo kwa sababu ni muhimu kwa kila mmoja kuwa sehemu ya uamuzi utakaofikiwa na kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wa maazimio ya baraza hilo kwa pamoja na kwamba huo ndio uwajibikaji wa pamoja.

"Nikiwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na kiongozi wa juu serikalini, naomba pia nizungumzie suala la maadili, uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma kuwa ni msingi wa utumishi ulitukuka ambao wananchi ndio wanautegemea kutoka katika taasisi za umma," alisema.

## Waziri akemea sheria mkononi

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, amewataka wananchi kuacha kujichikulia sheria mkononi na badala yake watumie mahakama.

Mkuchika aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa jengo la mahakama lililogharimu Sh. milioni 679.

Alisema mhimili pekee unaoweza kutenda haki baina ya watu ambao wameshindwa kuelewana ni mahakama pekee, hivyo watu waitumie kupata haki.

"Nawaomba mtumie jengo hilo kutafuta haki na masuluhisho mbalimbali na si kujichukulia sheria mkononi," alisema Mkuchika.

Naye Waziri Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alisema wana kila sababu ya kuipongeza serikali kwa ujenzi wa jengo hilo.

Alisema jengo hilo liwe chachu ya wafanyakazi kutenda kazi kwa ufasaha ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake ya msingi.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mathias Kabundugulu, alisema ujenzi wa jengo hilo ni moja ya miradi 16 ambayo inatekelezwa nchini.

Alisema pia wanatarajia kujenga jengo lingine la mahakama eneo la Kibaigwa, Kongwa mkoani Dodoma.

Naye Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema, wamefanya utafiti wa miaka mitano kuona wapi mahakama inapaswa kujengwa, kukarabatiwa na kusimamiwa.

# Madaktari bingwa Cuba kutua nchini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamini Mkapa imetia saini mkataba wa makubaliano na Cuba kwa ajili ya kupata madaktari bingwa saba ambao wataungana na madaktari bingwa wa hospitali hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutiliana saini mkataba huo wa kupata wataalamu na madaktari bingwa kutoka nchini humo. Alisema lengo kubwa la mkataba huo ni kuongeza ufanisi wa kitabibu huku akieleza wazi kuwa Cuba na Tanzania ni nchi marafiki toka enzi za baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.


"Leo (jana) ni siku ya kihistoria hapa nchini tukiwa na Balozi nchini Tanzania kutoka Cuba. Ni siku ya kuingia makubaliano baina ya Hospitali ya Benjamini Mkapa na wenzetu kutoka Cuba kwa lengo la kupata wataalamu na madaktari bingwa pamoja na wauguzi," alisema Dk. Chandika.

Alisema kitendo cha wataalamu kutoka Cuba kuja Tanzania kitawapatia uzoefu na kuwafundisha baadhi ya wataalamu wa hospitali hiyo na kuwapa ujuzi wa matumizi mazuri ya vifaa vya kisasa ambavyo vimesheheni katika hospitali hiyo.

Pia alisema Cuba ni nchi ya watu ambao wamebobea katika masuala ya kitabibu na hawana gharama kubwa tofauti na kuwatafuta wataalamu wengine.

Aidha, Dk. Chandika alisema Cuba imekuwa na wataalamu ambao wamefanya kazi ya matibabu katika maeneo mbalimbali na wale ambao wanakuja katika hospitali hiyo ni madaktari wa kiwango cha juu zaidi ambao watashirikiana na wataalamu wa ndani kuwapatia utaalamu.

Katika hatua nyingine Dk. Chandika alisema wataalamu hao saba watakuwa wamegawanyika katika maeneo mbalimbali ikiwamo maabara ya moyo, uchunguzi wa mfumo wa chakula, utumbo mpana na upasuaji. Alisema wengine kuwa ni wataalamu wa chumba cha wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU), kitengo cha majeruhi, upasuaji ubongo, dawa za usingizi na watashirikiana na wa madaktari wazawa kuwapa uzoefu wa utumiaji wa vifaa vya kisasa.





Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir (wa tatu kulia), akitoa tamko la viongozi wa vyama kumi vya siasa Tanzania la kupongeza mafanikio ya miaka tisa ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar yajizatiti kudhibiti corona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kukabiliana na virusi hatari vya corona vinavyosababisha homa kali inayoambatana na mafua, vilivyoripotiwa kuua mamia ya watu China.

Imesema imechukua hatua kufuatia kuripotiwa kwa zaidi ya mataifa 10 ulimwenguni kuthibitisha kutokea kwa kesi za maambukizo ya virusi hivyo.

Timu ya Wizara ya Afya Zanzibar ikiongozwa na Katibu Mkuu wake, Asha Ali Abdulla, ilitoa kauli hiyo kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi baada ya kumaliza mazungumzo yao na madaktari bingwa wa taasisi ya kuhudumia maradhi ya moyo kwa watoto (SACH) ya Israel.

Asha alisema kinachozingatiwa zaidi kwa wakati huu ni kwa wataalamu wa afya kujipanga kutoa elimu itakayowasaidia wananchi kukabiliana na virusi vya corona. Alisema wakati jitihada hizo zikiendelea taasisi, mashirika, jumuiya za kiraia na wananchi wanapaswa kubeba jukumu katika kuhakikisha suala la utunzaji wa mazingira ili kujiepusha na maambukizo ya maradhi mbalimbali yanayoikumba jamii.

Akizungumza na madaktari bingwa kutoka SACH, Balozi Iddi alisema mfumo wa wataalamu hao kuja nchini kutoa huduma za matibabu ya moyo unatoa fursa kwa wagonjwa wengi kupata huduma hiyo muhimu.

Alisema wananchi wengi hasa wale wenye kipato cha chini wamefaidika na mfumo huo kwa kupunguza gharama za matibabu ya kuwapeleka nje ya nchi wagonjwa.

Balozi Iddi aliushukuru uongozi wa taasisi hiyo kutoka Israel kutokana na huduma inazotoa zinaendelea kuleta faraja kwa wananchi walio wengi nchini.

Alikumbusha umuhimu wa kuongeza ushirikiano kati ya mabingwa hao wa Israel na madaktari wazalendo ili kufanikisha kazi hiyo muhimu inayogusa maradhi yanayohitaji umakini wa hali ya juu yakiwa pia na gharama kubwa.

Kiongozi wa SACH, Dk. Mara Chapira, alisema timu yake inatarajiwa kuwafanyia uchunguzi watoto wapatao 400 katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ambao wanasumbuliwa na maradhi ya moyo.

Alisema watoto watakaobainika kuwa na sababu za kufanyiwa huduma za upasuaji, utaratibu wa kuwasafirisha kwenda Israel utapangwa kama ilivyokuwa vipindi vilivyopita.

# ACT yatamba ushiriki wanawake uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kimejipanga vizuri kuona wanawake wanashiriki kikamilifu katika uchaguzi wa ndani ya chama na uchaguzi mkuu mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake wa ACT-Wazalendo, Zahra Hamad, alisema jana kuwa fursa ya wanawake kushiriki katika harakati za uongozi kupitia chama cha ACT-Wazalendo ni kubwa.

"Hakuna vikwazo kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali... tumeweka asilimia 30 ambayo wanawake wanatakiwa kuifikia katika ngazi za uongozi'," alisema.

Aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Fatma Fereji, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za uongozi katika chama cha ACT-Wazalendo na hakuna vikwazo vya kuwazuia.

Alisema wanawake wanayo nafasi ya kuwania nafasi za uongozi kupitia ngome ya wanawake, lakini kupitia jumuiya nyingine katika ngazi za mashina hadi taifa.

Fereji alisema kitendo cha wanawake kuwania nafasi za uongozi kupitia chama hicho ni moja ya fursa kubwa ya kuweza kupata nafasi hizo ikiwamo nyadhifa za uwaziri katika serikali ya umoja wa kitaifa.

"Wanawake hawawezi kupata nafasi za uongozi ikiwamo uwaziri kama hawatachukuwa fomu kuwania nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali ikiwamo majimbo ya uchaguzi," alisema.

Mmoja ya mwanachama wa chama cha ACT-Wazalendo, Asiya Mohamed, alisema amejipanga kuwania uongozi kupitia uwakilishi katika majimbo ya uchaguzi ya Zanzibar.

Alikitaka chama kutoa nafasi kwa wanawake ikiwamo wale ambao wamepata kura nyingi za maoni kufikiriwa na kuacha kutoa kipaumbele zaidi kwa wanaume.

"Tunakiomba chama chetu kutufikiria zaidi wanawake katika nafasi za uongozi kupitia majimbo ya uchaguzi kwa sababu wanawake ndiyo wapigakura wakubwa wenye ushawishi kwa wananchi," alisema.

# Wataka usafirishaji urasimishwe

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WADAU wa sekta ya usafiri na usafirishaji barabarani wametaka kuanzishwe kwa utaratibu wa kurasimisha sekta hiyo izidi kuchangia na kukuza uchumi wa taifa.

Wakitoa ushauri na kupendekeza hatua za baadaye za kufuatwa katika kufanikisha suala hilo katika mkutano wa wadau kutoka sekta mbalimbali za usafiri barabarani, wadau hao walisema wizara inayoshughulika na masuala ya kazi, inapaswa kuandaa utaratibu wa kisheria na kutayarisha mikataba ya kazi.

Walisema utaratibu huo utasaidia kuingia katika sekta hiyo bila vikwazo vingi katika hatua ya urasimishaji kamili wa sekta hiyo.

Wadau hao wakiwamo watendaji wa idara ya usafiri na leseni, Jeshi la Polisi, Bodi ya Mapato ya Zanzibar, Kamisheni ya Kazi pamoja na wamiliki wa vyombo vya usafiri barabarani, walisema kila mdau kuelimishwa faida na vikwazo katika urasimishaji huo ili wapate uelewa na ufanisi mzuri.

Suleiman Samba kutoka idara ya usafiri na leseni, alisema ni vyema kuwatambua na kusajili taasisi zitakazofanya kazi ya kushughulikia huduma wakati sekta hiyo itakaporasimishwa rasmi na serikali kwa faida ya mwajiri, mwajiriwa na wananchi kwa ujumla.

Wadau waliitaka serikali kuanza kufikiria aina ya magari ambayo yatahitajika au kufaa kufanya kazi katika utaratibu huu wa urasimishaji wa sekta hii ya usafiri barabarani.

Pia, walipendekeza kuundwe kamati maalum ya wadau ya kusimamia masuala hayo kwa ufanisi na kuchangia uchumi wa taifa.

Akitoa maelezo ya kikao hicho, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira katika Wizara ya Kazi, Ali Suleiman Ameir, alisema kutokana umuhimu wa urasimishaji huo, sekta hiyo italeta ufanisi na tija zaidi kwa pande zote na lengo la kuimarisha ajira za staha na kukuza uchumi wa mwananchi na taifa litafikiwa nchini.



**BEKA**

Soma UK.14

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI FEBRUARI 1, 2020




# YOTE NI WIVU

## WALIMTOKEA KIMAPENZI, AKAWATOLEA NJE

Soma UK.14

## BASI SAWA



### Sauti ya Busara kurindima Februari 13

KUNDI la muziki wa kizazi kipya, The Mafiki na rapa Wakazi watapamba jukwaa la Tamasha la Muziki la Sauti ya Busara linalotarajiwa kufanyika kwa siku nne kuanzia Februari 13 hadi 16 mwaka huu.

Tamasha hilo kwa mwaka 2020 litakuwa na wasanii kutoka nchi tofauti tofauti ambao watatoa burudani yenye ladha za kiasili.

"Nimefurahi ni 'opportunity' nzuri kwangu mimi, nitaweza kuonesha kile nilichonacho na nafasi ya kujifunza mengine kutoka kwa wasanii mbalimbali na naendelea kujipanga mpaka siku itakapo fika" alisema Wakazi.

"Hii ni mara yao ya kwanza toka kundi limeanza kama The Mafik, tuliomba kati ya waliotuma maombi wao wakachaguliwa baada ya vigezo vyao kuonekana vimekizi wao kuwapo kwenye hili tamasha la Sauti za Busara wakachaguliwa, hili ni dili lao kubwa sana toka nimeanza kuwasimamia." – Meneja The Mafik.




### Beka Flavour hana shida kivile

MSANII nyota wa Bongo Fleva, Beka Flavour, amesema katika maisha yake ya muziki nje ya Yamoto Band, hajawahi kupiga simu ya kuomba msaada kwa wasanii wenzake waliokuwa wakiunda kundi hilo.

Beka ambaye ametambulisha kibao chake kipya 'Again' amesema yeye na wenzake bado wana uhusiano mzuri, lakini hajawahi kufanya hivyo kwa sababu hana tatizo la kifedha au kutungiwa nyimbo.

"Nikimpigia simu Aslay au Mboso nitawaambia tu wanisaidie kusukuma kazi yangu na si vinginevyo, naamini sisi wote bado tunapendana na ndio maana tunaendelea kuwa pamoja," amesema Beka.




## YOTE NI WIVU

## WALIMTOKEA KIMAPENZI, AKAWATOLEA NJE

MKALI wa muziki wa RnB, Ben Pol, ameibua mjadala mkali baada ya kudai anaonewa wivu kutokana na kuwa na mwanamke mzuri na ambaye amembadilisha maisha yake.

Akipiga stori na EATV na EA Radio Digital, Ben Pol kuzungumziwa kwake inatokana na mpenzi wake kuwa mzuri, licha ya uwezo wake wa kifedha aliokuwa nao.

"Kwanza nadhani watu hawajanizoea kuweka mahusiano yangu hadharani, kwa hiyo imeleta mitazamo tofauti, pili mpenzi wangu anaongelewa kiupande wake kwa kule kwao na hata huku kuna Watanzania ambao walikuwa wanamfuatilia kwa muda mrefu, halafu ni mtu maarufu na kitu kingine ni mzuri," ameeleza Ben Pol.

Akizungumzia juu ya tuhuma ya kubadilishwa kimaisha na mpenzi wake raia wa Kenya Anerlisa Muigai, amesema, "Ameniweka karibu na Mungu zaidi, ameniongezea utu na ubinadamu wa kawaida, ananisaidia katika mawazo ya kazi, ana sikio zuri la muziki, jicho la fashion, na tunasaidiana kwenye kazi zetu."

## INSTA-TWITTER





**Unapopata** nafasi ya kumjali na kumthamini mtu, fanya kwa moyo wote. siyo mpaka umpoteze ndiyo ukumbuke kumthamini na kumpenda - **Shamsa Ford.**



**Usipekue** simu ya mpenzi wako kabla haujajiandaa kufanya maamuzi- **Gago Zigamba.**



## Linex amshukuru mpenzi aliyemuacha

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Linex Sunday Mjeda, ameibua mjadala baada ya kumshukuru mpenzi wake wa zamani kwa kueleza kitendo chake cha kumuacha kilimpa mafanikio katika muziki.

Ameiambia Planet Bongo ya East Africa Radio, kwamba asingeachwa na mwanamke huyo asingejua hatima yake kama angekuwa wapi hadi leo.

"Popote ulipo Halima nakushukuru sana kwa sababu kunitupa kwako kulisababisha niandike wimbo mzuri ambao utafanya uishi milele, hata kesho nikiwa sipo watu watasikiliza, nakubaliana na kuniacha kwako, sio lazima kila mtu awe adui yako na asingeniacha sijui leo hii ningekuwa wapi mimi, ahsante mama," ameeleza Linex.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**



# HAFSA KAZINJA KUTAMBULISHA 'KWA YESU HAKUNA PRESHA'

MWIMBAJI wa injili, Hafsa Kazinja ambaye kwa sasa anatambulika kwa jina la Christine Kesho, anatarajia kuipua albamu mpya aliyoipa jina 'Kwa Yesu Hakuna Presha'.

Akizungumza na BT, Kazinja amesema albamu yake hiyo ya kwanza baada ya kuamua kuokoka, itazinduliwa kwenye ukumbi wa Kanisa la Mchungaji Ado Novemba lililopo Sinza Mapambano.

Amesema miongoni mwa nyimbo zilizopo kwenye albamu iyo ni 'kwa Yesu hakuna presha' ambao ameubadili maneno ya nyimbo yake ya awali wa Presha aliyoshirikiana na Banana Zorro ambao ulimpa umaarufu katika Bongo Fleva.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Mwezi** Januari ulikuwa mrefu sana jamani, hivi shida ilikuwa wapi?-**Juma Lokole.**



**Hivi** ulishawahi kusubiri simu ya mpenzi wako mpaka ikabidi ufungue simu kuangalia kama line imekaa vizuri? - **Chuchu Hans.**



**Mimi** ndiyo msanii wa kwanza kufunga ndoa 2020, na nitakuwa msanii wa kwanza ambaye ndoa yake itavunjikia kaburini. Tutafurahia mpaka kuzimu, yaliyotokea kwa Stamina na Mabeste nimejifunza kuwa makini na nimpende sana mke wangu tusije kuachana - **Peter Msechu.**

# Kuumbe!




# STARA FASHON WEEK

## JUKWAA LA MAVAZI NA UTUNZAJI MAZINGIRA

TAMASHA la sita la mavazi la Stara Fashion Week 2020, linatazamiwa kufanyika Aprili 17 na 18 jijini Dar es Salaam.

Kufanyika kwa tamasha hilo itakuwa wiki moja kabla ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Katika siku hizo za maonyesho ya mavazi, jumla ya wabunifu 30 watashiriki pamoja na wadau wengine wa mavazi wakiwamo wafanyabiashara na wajasiriamali.

Kwa mujibu wa waandaji wa tamasha hilo, Latifah Makau, amesema kaulimbiu ya mwaka itakuwa ni 'Fashion na Utunzaji wa Mazingira'.

"Sekta ya mavazi inatajwa kuwa msababishaji mkubwa wa uchafuzi wa mazingira duniani, na kwamba jukwaa hili la fashion lijulikanalo kama Stara, limeona umuhimu wa kuwahusisha wabunifu kufikiria kujipanga kuonyesha uwezo wao kupitia mabaki mali.

Amesema kuanzisha kampeni hiyo itakuwa ni vita dhidi ya uchafuzi wa mazingira kupita mitindo.

"Baada ya hapo tutakuja na suluhisho ya nini kifanyike kukabiliana na takataka zinazozalishwa na mafundi baada ya mavazi kushonwa," ameongeza kusema Latifah.

Pia katika jukwaa hilo, wabunifu watajifunza namna ya kujiongezea kipato kupitia mabaki yanayozalishwa katika kazi zao.

Pia watu watakaohudhuria licha ya kupata fursa ya kuangalia mitindo mipya ya mavazi, pia watapata burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya.

"Mkakati huu utakuwa endelevu na itakuwa kama sauti yetu ya kutoa wito kutaka hatua zichukuliwe." anasema Latifah.

Uzinduzi wa msimu mpya wa Stara Fashion unatazamiwa kuchukua nafasi yake tarehe 29 Februari katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam na baada ya hapo warsha na semina mbalimbali zitaelekea kuelekea kilele cha tamasha hilo.





# Hata zamani michepuko ilitingisha

**Na Adam Fungamwango**

INADAIWA kwa miaka ya sasa kuna ongezeko kubwa la usaliti kwenye mapenzi au ndoa, kwani tunashuhudia idadi kubwa ya wapenzi au wanandoa wakiachana kwa sababu hiyo.

Wanaume wamekuwa wakitoka na wanawake wengine wakiwa ndani ya ndoa, wakiwa na wachumba au wapenzi wao. Wanawake pia nao wamekuwa wepesi kuchepuka na kutoka nje ya ndoa, au hata ana mchumba anayetaka kumuona au mpenzi wake wa kudumu, bado anakuwa na mwingine wa pembeni.

Hii imesababisha wengi kuchukia ndoa, au kutaka kuwa peke yao bila mpenzi.

Hata hivyo, imebainika kuwa jambo hili liko tangu zamani, enzi na enzi za mababu zetu.

Kinachotakiwa siyo kuacha kuoa au kuolewa, ila ni watu kuishi kwa hofu ya Mungu, kufanya sala na kumuomba aepushe mabaya yote.

Wakati kwa sasa tunashuhudia usaliti wa mapenzi, watu wakiachana kila kukicha, mastaa pamoja na umaarufu wao wakishindwa kulinda ndoa zao na sasa kukiwa na nyimbo nyingi za usaliti wa mapenzi, kumbe suala la watu kuchepuka ilikuwapo tangu miaka ya nyuma.

Ukitaka kuthibitisha hili, hebu angalia nyimbo hizi za zamani ndiyo utajua kuwa kinachowapata watu leo hii, kiliwapata wengine huko nyuma.

**Edita-DDC Mlimani Park**

Edita ni wimbo uliopigwa na bendi ya DDC Mlimani Park. Maudhui yake ni kwamba jamaa anamtimua mpenzi wake baada ya kumfumania nyumbani kwake akiwa na mwanaume mwingine.

Anamwambia kuwa aliambiwa na majirani siku nyingi kuhusu tabia yake, lakini alidhani ni fitina tu, lakini leo ameamini kwani amemfuma laivu.

Anamwambia ndiyo maana kila akirejea nyumbani hamkuti, na akirudi anamwambia alikuwa kwa shangazi Kariakoo, kumbe anakwenda kwa bwana 'ake. Lakini haikutosha, sasa ameamua amlete hadi nyumbani hapo wanapoishi. Mwisho anamwambia achukue kila chake aondoke.

**Milima ya Kwetu-Super Rainbow**

Wimbo huu ulitungwa na marehemu Eddy Sheggy, akiwa na Super Rainbow. Mtunzi anarejea kwao Lushoto, akiwa anaitazama milima ya kwao. Akiwa ndani ya basi anakumbuka siku alipotoka kwao Lushoto kwenda Dar alikuwa na mkewe, lakini sasa anarejea peke yake. Atakwenda kuwaambia nini wazazi, ndugu na marafiki? Nini kilitokea wakiwa Dar.

Ni kwamba baada ya kufika Dar, mkewe akachangamka. Akawa anajua zaidi kuliko mumewe. Akawa mtoto wa mjini. Kila bwana wa kwake. Akaanza kumfanyia visa mumewe. Hali ikawa mbaya mpaka mwanamke akatoroka na kumuacha mumewe akiwa hana la kufanya.

**Baba Jenny - Hamza Kalala na Bantu Group**

Hamza Kalala alitunga wimbo wa 'Baba Jenny', akisimama kama mwanamama anayelalamika kuhusu visa vya mumewe.

Mama huyo anadai kuwa gari la mumewe hajawahi kupanda hasa siku moja, zaidi ya kulijua kwa honi, kukosha na kufuta vumbi, pamoja na muungurumo.

Gari hilo linatumika zaidi kumbeba kimada wa mumewe na kwenda naye kwenye starehe.

Mbaya zaidi ni siku moja mumewe alipompita kwenye kituo cha basi akiwa na watoto mvua kubwa inanyesha, lakini jamaa ndani ya gari alikuwa na kimada wake akawapita kama hawajui.

Mwisho anamuaga mumewe bai bai, yamemfika shingoni, anaondoa, siyo kama hampenzi, lakini tabu zimezidi.

**Stendi ya Basi-Orchestra Tomatoma**

Ukitaka kujua kuwa watu walikuwa na wasiwasi wa wake au waume zao kuchepuka sikiliza kisa hiki kwenye wimbo wa 'Stand ya Basi'.

Hapa mume anamuuliza mkewe kuwa kila siku anarudi usiku kutoka kazini, halafu hakuelewielewi, sababu ni nini hasa?

Mke anamjibu kuwa anachelewa stendi ya basi, kwani kuna tabu sana ya mabasi na hakuna asiyejua hilo.

Ikumbukwe kuwa miaka ya '80 hadi mwanzoni mwa '90 Dar ilikuwa na tatizo la usafiri, lakini kwa sasa kama kweli huyo dada anachelewa kwa mchepuko, angeweza kumdanganya mumewe kuwa anachelewa kwa sababu ya foleni.

**Baba Shaaban-Juwata Jazz band**

Ulikuwa ni utunzi wa marehemu Shaaban Mbwembwe, ukimzungumzia mwanamama mmoja akimuuliza mumewe anasikia kwa majirani kuwa ana mchepuko huko nje anayempenda sana.

Mumewe anamjibu kuwa asiwasikilze kwa sababu nia yao wanataka watengane ili wawacheke na hizo zote ni fitina za maisha yao mazuri kuliko ya kwao.



# IMETOKEA

## Takabuti binadamu aliyeishi miaka 2,600

TIMU ya wataalamu imepata ufumbuzi wa kile kinacholeta mkanganyiko kwa miongo mingi kuhusu maiti ya kale ya Misri ilifikaje makumbusho ya Ulster? Kulingana na utafiti uliofanywa kwa njia ya kisasa zaidi, iligundulika kuwa 'Takabuti' mtu huyo aliuawa kwa kudungwa kisu mgongoni.

Wataalamu hao pia wanaamini kwamba huenda hata maiti hiyo asili yake siyo Misri, kulingana na uchunguzi wa vinasaba, jeni zake zinafanana zaidi na Ulaya ikilinganishwa na Misri ya sasa.

Uchunguzi uliofanywa kwa teknolojia ya kisasa na hata kisayansi umetoa ufumbuzi wa kifo cha maiti hiyo ambayo ilipelekwa Belfast mwaka 1835.

Matokeo ya uchunguzi huo yametolewa kwa umma katika karne ya 185 tangu alipokufa.

Profesa Rosalie David, mtaalamu wa vitu vya kale vya Misri kutoka chuo kikuu cha Manchester, amesema utafiti umetoa ufafanuzi wa kina wa Takabuti na historia ya wakati alipokuwa hai.

"Ugunduzi ambao haukutarajiwa na wa msingi katika historia ya Ulaya, umekuwa ufumbuzi wa aina yake katika historia ya Misri," amesema.

"Utafiti huu ambao ulihusisha teknolojia ya kisasa ya sayansi katika maiti za kale za Misri unaonyesha taarifa mpya inaweza kupatika miaka elfu kadhaa baada ya kifo.

"Timu yetu inayojumuisha taasisi na wataalamu ilikuwa katika nafasi ya kipekee ya kushirikishana utaalamu wao na teknolojia kwa utafiti mpana wa namna hii."

Profesa Eileen Murphy, mtaalamu wa mabaki ya binadamu kutoka chuo kikuu cha Queen huko Belfast, ameelezea matokeo ya utafiti huo kama kitu cha kustaajabisha.

"Awali mara kwa mara Takabuti alisemekana anaonekana mwenye amani akiwa kwenye jeneza lakini baada ya utafiti huu tumebaini kuwa muda wake wa mwisho alipitia madhila makubwa kwa sababu aliuawa."

Mwaka 2009, makala ya BBC Ireland Kaskazini, ilionyesha vile ambavyo Takabuti angelionekana.

Pia utafiti huo uligundua vitu kingine cha ajabu mwilini mwake. Vitu hivyo vinasemekana kwamba vilitumika kuziba jeraha la kisu alilopata huku moyo wake ukipatikana na kwamba upo katika sehemu stahiki.

Takabuti aliishi Thebesi wakati wa utawala wa 25 karibia miaka 2,600 iliyopita.

Baba yake, Nepare, alikuwa kasisi katika hekalu la Amun, Karnak na mama yakeTasenirit, alikuwa kijakazi.

Inaaminika kwamba Takabuti alikuwa ameolewa kwa sababu alikuwa kimada wa Thebesi.

Aliaga dunia akiwa katika umri wa miaka ya 20 na kuzikwa karibu na hekalu la Hatshepsut.

Takabuti aliga dunia baada kudungwa kisu mgongoni.

Mama yake Takabuti alikuwa mwenye asili ya Ulaya au Mzungu. Hata hivyo, kwa utafiti wa hivi karibuni, hakuna uhakika kwamba Takabuti alikuwa ni raia wa kigeni nchini Misri.

Bado moyo wake upo, japo utafiti wa awali haukufanikiwa kubaini hili.





## Nzowa Damu ya mtu haipotei

**Na Adam Fungamwango**

MAISHA ni safari ndefu. Na kwenye safari kuna mengi ya kushtua, kushangaza, kuhuzunisha na kusikitisha. Safari ya maisha inaweza kuwa ndefu sana, yenye milima na mabonde na vikwazo chungu nzima kiasi cha kukatisha tamaa. Lakini kuna siku isiyo na jina yote yataisha na kubaki historia itakayosimuliwa vizazi na vizazi.

Filamu ya Nzowa inathibitisha maelezo haya. Ni filamu yenye huzuni kubwa ukiitazama, lakini yenye mafunzo ya hali ya juu kwenye maisha, na hasa kwenye jamii yetu hivi sasa iliokosa utu.

Imechezwa na wasanii Tino Muya, Mashaka (marehemu), Sajuki (marehemu), Wastara na wengineo.

Picha linaaza kwa kuonyesha Natasha akiwa anamuuguza mgonjwa ambaye ni mumewe Mashaka. Mashaka ni mwanaume ambaye hana mtoto, lakini ana mali nyingi. Mashaka alimchukua Natasha ukubwani na kuamua kuishi naye, kwani hakuweza kuishi peke yake uzeeni.

Natasha ambaye alikuja kuishi na Mashaka akiwa na kijana wake Sajuki. Akili ya Natasha na kijana wake Sajuki ilikuwa kwenye mali tu na si vinginevyo.

Mashaka alivyoanza kuumwa walifurahi wakijua kabisa sasa ni wakati wa kumiliki mali.

Kwenye nyumba hiyo kuna wafanyakazi wawili, Wastara ambaye ni hausigeli na Tino ambaye ni hausiboi.

Tangu Tino aliyetumia jina la Nzowa aanze kazi pale na kupewa kazi ya kumhudumia mgonjwa Mashaka, hali yake ilianza kutengemaa.

Hilo liliwakasirisha Natasha na kijana wake. Wakaanza kumchukia Nzowa na kumfanyia kila aina ya vitimbi, kama vile kunyanyasa na kumpiga.

Hilo lilimuuzunisha Wastara ambaye alikuwa hana la kufanya. Natasha anatumia hata njia ya kumpelekea karatasi mgonjwa ili asaini kuwa kama akifa mali ziwe zake, lakini mgonjwa anakataa.

Mwanasheria na daktari wa mzee Mashaka aliyetumia jina la Bangusilo, walionekana kupendezwa na uwajibikaji wa Tino na kutokea kumwamini, hivyo kila wakija mtu waliokuwa wakiongea naye na kumpa dawa za mgonjwa ni yeye pekee.

Siku moja mwanasheria alikaa na Tino na kumuuliza ametokea wapi? Tino akamwambia yeye ni yatima aliyeokotwa tu mitaani, na anaambiwa historia yake ni kwamba mama yake alipachikwa mimba na baba aliyejulikana na kusababisha afukuzwe nyumbani, akajifungulia ufukweni mwa bahari, kabla ya kufariki na yeye kulelewa na wasamaria wema, baadaye aliingia mitaani, kabla ya kukutana na mama wa nyumba hiyo.

Mgonjwa aliishiwa damu. Mkewe Natasha na Sajuki, walikataa katakata kutoa damu, lakini Wastara na Tino ambaye ni wafanyakazi wa ndani wao ndiyo walijitolea, hivyo daktari akachukua damu zao.

Mgonjwa alipata nafuu alirejea nyumbani na kuendelea kutumia dawa zake alizokuwa akipewa na Tino.

Hilo lilimpa nafasi Sajuki kutia sumu kwenye dawa za mgonjwa baba yake wa kambo.


Tino alipompa dawa mgonjwa akafariki na alikamatwa mara moja kwa kosa la kuua kwa kumpa sumu mgonjwa tena kwa makusudi.

Wakati akipata mateso makali ili akiri kosa, Wastara anaingia kwenye kituo cha polisi na kuwaambia kuwa alimuona kwa macho yake Sajuki akitia sumu kwenye chupa ya dawa ya mgonjwa.

Polisi walimuachia Tino na kumkatana Sajuki ambaye baada ya kubanwa akikiri na kusema kuwa alitumwa na mama yake mzazi Natasha. Natasha naye baada ya kutiwa mbaroni akamsingizia mtoto wake. Lakini wote lao lilikuwa moja. Wakahukumiwa kwenda jela maisha.

Daktari alimfuata Tino na kumwambia kuwa alipima damu ya mgonjwa kabla hajafa na yake kwenye vipimo vya DNA alipochukua kwenda kumwekea damu mgonjwa na kugundua kuwa ana nasaba ya marehemu mzee Mashaka, hivyo ni baba yake mzazi.

Taarifa hiyo ilifikishwa na mwanasheria wa mzee Mashaka na kuamua kumrithisha Tino mali zote za marehemu mzee huyo, wakati Natasha na kijana wake Sajuki wakitumikia kifungo cha maisha jela.



# MASTAA WANAPOANGUKA

## MILEY, LIAM WAPEANA MIKONO YA KWAHERI

NDOA nyingine inayowahusu mastaa nchini Marekani, Miley Cyrus na Liam Hemsworth, imevunjika rasmi.

Kulingana na mtandao wa TMZ, imebainika kwamba wanandoa hao wameachana rasmi baada ya mahakama kukubali kutoa talaka baada ya mwafaka kutopatikana.

TMZ imeeleza kwamba Laura Wasser ambaye ni mwakilishi wa mawakili wa Liam na Judith R. Forman, wakili wa Miley Cyrus, wamekubaliana kutolewa kwa talaka hiyo mbele ua jaji.

Moja ya nyaraka inasema Miley Cyrus na aliyekuwa mume wake watakuwa wakitunza wanyama wao wote na itakuwa rahisi kwao kushirikiana bila shida yoyote.

Mgogoro ulianza mwaka 2019 baada ya wanandoa hao kuanza kutoa siri kwamba hawana uelewano kama mume na mke.

Itakumbukwa kwamba Liam alitangaza Agosti 2019 kwamba amelipa gharama ya talaka, jambo linaloonesha kwamba tofauti zao haziwezi kupata suluhu.

Hata hivyo, haikuchukua muda mrefu uvumi ukaenea kwa kasi kuwa alidanganya.

Nyota huyo mwenye talanta nyingi akaibuka na kupinga uvumi huo na kueleza kwamba ndoa yake ipo katika hatihati ya kuvunjika.

Nyota huyo wa muziki alitangaza kupitia ukurasa wake alisema kuwa sasa ni mwanamke mtu mzima ambaye amewajibika kwa matendo yake.

Akisisitiza kwamba uamuzi wa kujitenga kutoka kwa Liam ulikuwa kwa faida yake.

Miley alionekana kumbusu Kaitlynn Carter wakati alipokwenda safari ya mapumziko nchini Italia, baada ya kupita saa 24 tangu kuzagaa kwa habari ya kujitenga kwake.

Cyrus na Carter, 30, walionekana wakila bata huko Los Angeles, na wapashaji habari wakisema kwamba walikuwa wapenzi.


# Sauti Sol walamba dume UMG



KUNDI la muziki la Sauti Sol, limesaini mkataba wa kufanya kazi na lebo ya kimataifa ya Universal Music Group (UMG) Afrika.

Universal Music Africa ni tawi la Universal Music Group (UMG), ambayo ni lebo kubwa ya uzalishaji muziki duniani na mkataba huo utakuwa mafanikio makubwa kwa kundi hilo kutoka Kenya.

Sauti Sol inaundwa na wasanii kama Bien-Aimé Baraza, Willis Chimano, Savara Mudigi na Polycarp Otieno.



## Toyin kwa hili umeeleweka

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Toyin Abraham, amewashauri watu wasihukumu mambo yaliyopita, badala yake waangalie mbele.

Akitumia akaunti yake ya Instagram, Toyin, ameandika kwamba kila mtu ana mambo mengi aliyofanya nyuma, si vizuri kuhukumu na kuyakumbuka.

"Kila mmoja ana mambo ya nyuma, baadhi yanakuwa makubwa kuliko mwingine, usijaribu kuhuku ya nyuma kwa sababu huwezi kujivuni," ameandika Toyin.

## Toke umesema kuntu, wamekusikia

STAA wa filamu wa Nigeria, Toke Makinwa, amesema watu wanaamini katika mila na tamaduni talaka ni moja ya sehemu inayosababisha kilio kama mtu aliyeua.

Toke akitumia ukurasa wake wa Twitter, alijaribu kuweka hisia yake hiyo wakati akijadili kisa cha msichana mmoja, Maryam Sanda, ambaye anadaiwa kumuaa mume wake siku chache baada ya ndoa.

"Wanasema talaka sio chaguo wala alama ya kwenda kinyume na tamaduni zetu, lakini ukifa au kuua kwa sababu ya njaa, watu ndipo wanasema utalia kwa ajili ya maisha yako," amesema.





## Mashabiki wa Burna Boy mwachieni Mungu

MASHABIKI wa mwanamuziki nyota wa Nigeria, Burna Boy, wametakiwa kutulia kwa sababu hakuna hujuma iliyofanyika kumwangusha katika utoaji tuzo za Grammy 2010.

Shade Ladipo, amesoma kukosa tuzo hiyo inatokana na uchanga wake katika muziki na ndio maana ilikwenda kwa mwanamama Angelique Kidjo.

Amesema Angélique Kidjo na Fela ni watu waliodumu katika tasnia hiyo kwa muda mrefu na muziki wao unajulikana na wengi.

## Khaligraph anaposema 'Yes Bana'

RAPA kutoka Kenya, Khaligraph Jones. ametambulisha ngoma yake mpya 'Yes Bana' ambayo inaelezea maisha halisi ya watu wa chini wan chi hiyo.

Katika nyimbo hiyo amemtaja mwanamitindo na mrembo wa mitandao, Huda jambo ambalo limezua mjadala mkali.

Video ya wimbo hiyo iliyotayarishi na Ricky Bekko imekuwa na ubora unaokubalika na kupendwa na mashabiki wake.



**MAKALA**



**MIONZI YA SHERIA**

# Jinai ya namna mbili za mauaji

Na John Juma
0716217615

TUMEKUWA tukisikia fulani amepatikana na hatia ya kuua bila ya kukusudia au ameua bila kukusudia. Je, unajua nini maana ya kuua bila ya kukusudia kisheria?

Mara ya mwisho, neno kuua bila kukusudia limesemwa sana baada ya hukumu ya katika kesi iliyohusu kifo cha mwanahabari Daudi Mwangosi. Yapo mengi ya kujua kuhusu kuua bila kukusudia.

Kifungu cha 195 Sura ya 16, Kanuni za Adhabu ndiyo inazungumzia kuua bila ya kukusudia.

Katika sheria, kuua bila ya kukusudia (manslaughter) kunatofautishwa na kuua kwa kukusudia (murder). Kuua bila ya kukusudia, ni pale muuaji anatenda kile kinachosbabisha kifo, lakini hakudhamiria kifo kitokee.

Kuua kwa kukusudia, kisheria ni pale mtu anatenda kinachofanya kifo kitokee akiwa amedhamiria. Kwa hiyo, utaona tofauti kubwa ya kuua kwa kukusudia na ile ya kuua bila kukusudia, ni dhamira, nia, au lengo.

Dhamira, nia au lengo likiwa ni kuua, basi huko ndiko kuua kwa kukusudia. Dhamira, nia au lengo likiwa sio kuua, lakini kwa bahati mbaya mtu akafa, basi hiyo itakuwa ndio inaitwa kuua bila ya kukusudia.

UTAJUAJE KUSUDIO? Yapo mambo yanayotazamwa na mahakama kujua, iwapo kulikuwapo dhamira ya kuua au haikuwepo. Kikuu kimojawapo kinachoangaliwa ni mazingira, kabla ya tukio, wakati wa tukio na baada ya tukio.

Kwa mfano 'A' alimkashifu 'B' kwa matusi mabaya, B akakasirika sana. Baadaye 'B' akaenda kwake akaja na panga ambalo alilitumia kumuua 'A.' Hapo 'B' atakuwa ameua kwa kukusudia, kwa sababu alisafiri kutoka eneo la tukio , akatembea mpaka nyumbani kwake, akatafuta panga na kisha akaanza safari ya kurudi, anamtafuta tena A, akampata ndipo akamuua.

Hatua zote hizo za kwenda, kurudi na kadhalika,. zinathibitisha dhamira, nia au lengo. Hakuna bahati mbaya inayopitia hatua hizo zote.

Lakini, ingekuwa palepale baada ya kukashifiwa kwa hasira akampiga na kumuua, ingekuwa kuua bila kukusudia kulikotokana na joto la hasira (heat of passion). Kwa hiyo, ushahidi wa mazingira ya matukio kama hayo ndio utaifanya mahakama iamue kama mtuhumiwa ameua kwa kukusudia au hakukusudia.

Upande unaosema aliua bila ya kukusudia, utaleta ushahidi kuonyesha mazingira ya tukio na upande unaosema alikusudia, nao utaleta ushahidi kuonyesha mazingira ya kusudi, nia au dhamira.

AINA ZA MAUAJI Kwanza, ni kuua bila kukusudia, lakini kwa tendo linalotokana na hiari (voluntary manslaughter). Hiyo ni pale ambao ni kweli kuwa fulani alidhamiria kumpiga mwenzake, fulani au alimsukuma, lakini hakutaka afe.

Kwa mfano, mzazi, anamchapa mwanawe kwa kosa fulani, lakini katika kumchapa mtoto anakufa. Au, askari anapiga bomu la machozi ili watu wakimbie, lakini katika kufanya hivyo, bomu linampata raia na kumuua. Hiyo ni aina ya kwanza ya kuua bila kukusudia.

Aina ya pili, ni kuua bila ya kukusudia. Kwa tendo ambalo si la hiari (involuntary manslaughter). Kwa mfano, breki za gari zinakatika na gari inamuua mtu. Au bunduki imeshikwa vibaya, inajifyatua na kuua mtu.

Ni matendo ya uzembe, lakini hayakutokana na hiari kama ilivyo unapoamua kumchapa mwanao.


Aina hizo zote mbili ni kuua bila ya kukusudia. Naomba kuwasilisha.



**KALAMU YA MWALIMU**

# Vyeti vya kuzaliwa, sare visiwe vikwazo uandikishaji wanafunzi

Na Reubeni Lumbagala



ELIMU ni haki ya msingi ya kila mtoto. Kutokana na umuhimu wa elimu kwa maisha ya mwanadamu, serikali na wadau wake, wameweka msisitizo wa kipekee kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anadahiliwa, ili kuanza masomo mara moja, akajipatiye maarifa, ujuzi na stadi kupitia ujifunzaji shuleni.

Safari ya elimu ya mtoto, inaanzia shule ya msingi ambako mtoto huanza darasa la awali au chekechea. Baada ya kuhitimu darasa la awali, mtoto huyo huanza darasa la kwanza na safari ya elimu ya mtoto huyo, inaendelea mbele kufikia elimu ya sekondari hadi ngazi ya juu.

Kutokana na gharama kubwa ya elimu, serikali imechukua uamuzi wa kizalendo bila malipo kuanzia elimu ya awali, hadi kidato cha nne.

Lengo ni kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bila kikwazo cha aina yeyote. Utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo ilianza kutekelezwa rasmi mapema mwezi Januari 2016.

Kwa sasa sera unaingia mwaka wa tano wa utekelzaji wake, tangu kuasisiwa na serikali ya Awamu ya Rais wa Dk. John Magufuli ma kumekuwapo ongezeko kubwa la uandikishwaji wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza kwa upande wa msingi, pia kidato cha kwanza kwa upande wa shule za sekondari.

Kumeibuka changamoto ya baadhi ya wazazi na walezi kukosa vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao, pamoja na ukosefu wa sare za shule za watoto wao.

Pamoja na umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa na sare za shule katika uandikishaji wanafunzi, Kalamu ya Mwalimu inaona vitu hivyo havipaswi kuwa vipaumbele vya msingi kwa shule.

Hiyo ni inapofika wakati wa kuwapokea wanafunzi kwa ajili ya kuwadahili shule za msingi na sekondari, kwani vinachelewesha kasi ya uandikishaji na hata kuanza ufundishaji wa wanafunzi shuleni.

Akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Bahi mkoa Dodoma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo, alipiga marufuku mwanafunzi kuzuiwa kuandikishwa darasa la kwanza, kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa.

Jafo alikuwa Bahi kukagua uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza na mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule za sekondari.

"Nimeona nitoe ufafanuzi kuhusu suala hili, kuwa cheti cha kuzaliwa ni haki ya kila mtoto, lakini isimzuie mtoto huyo kuanza shule, eti kwa sababu tu hajapata cheti hicho.

"Watoto wote wapokewe, waandikishwe na waanze masomo, huku wazazi wao wakiendelea na mchakato wa kuwatafutia vyeti hivyo," aliagiza.

Msisitizo wa Waziri Jafo unatokana na kupokea malalamiko kutoka maeneo mbalimbali, ambako baadhi ya maeneo, shule zimekataa kupokea na kuwadahili wanafunzi wa darasa la kwanza, kwa kisa cha walezi kukosa vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao.

Pia, kwa wanafunzi wanaojiunga darasa la kwanza na wale wa kidato cha kwanza, wanapaswa kuwa na sare za shule zinazotumika katika shule wanazojiunga nazo, ili kufanana na waliowatangulia shuleni.

Hilo ni kuhakikisha kila mwanafunzi anapata haki ya elimu pasipo kuchelewa masomo. Suala la wanafunzi kuanza masomo huku wakiwa na sare mpya za shule halipaswi kuwa kikwazo cha kukataa kudahili wanafunzi, kwani anaweza kuhudhuria masomo huku taratibu za kununuliwa sare za shule zikiendelea kufanywa na wazazi au walezi wake.

Serikali ya Wilaya ya Kinondoni, chini ya uongozi wa Mkuu wa Wilaya hiyo Daniel Chongolo, imepiga marufuku wanafunzi walioanza kidato cha kwanza mwaka 2020 kurudishwa nyumbani, kwa sababu ya kutokuwa na sare.

Ni agizo lililotolewa na mkuu wa wilaya katika hafla ya kuzipongeza shule na walimu waliofanya vizuri katika mitihani ya darasa la saba mwaka 2019 wilayani humo.

"Jambo la msingi kwa mwanafunzi ni kuripoti shule na kuwa na daftari na vifaa vya kujifunzia, sijui hana sare, viatu au jembe, hicho si kigezo cha kutompokea.

"Tumetoa ada ili kumfanya mwanafunzi mnyonge kupata elimu basi tusiweke vigezo vitakavyoendelea kuweka mazingira ya kubaguliwa, wapokelewe wapewe elimu," alisisitiza Chongolo.

Wazazi na walezi wanapaswa kuendelee na juhudi za kuwatafutia watoto wao vyeti vya kuzaliwa na kuwanunulia sare za shule, ili watoto wasome shule bila tatizo.

Pia, wanafunzi wana wajibu wa kusoma kwa bidii ili kutengeneza mustakabali mwema wa maisha yao ya sasa na ya baadaye.

● **Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko Wilaya ya Kongwa, Dodoma. Anapatikana kwa simu: (+255) 765 409249.**

# UN kutumia gia ya ubunifu kutibu changamoto duniani

## ■Kar kufaidi mradi nishati ya pombe

**Na Gaudensia Mngumi**

ZAMA hizi dunia inakabiliwa na changamoto nyingi za kimaendeleo yakiwamo mahitaji makubwa mfano chakula, misaada ya kibinadamu kwenye majanga, elimu, maji, tiba na ajira rasmi, hali hiyo inatoa msukumo mpya wa kutumia ubunifu pamoja na teknolojia kuleta ufumbuzi wa matatizo yanayoibuka kila leo.

Zinaweza kuitwa zama za kuacha mazoea na kujikita kwenye ugunduzi na ubunifu ili kuleta majibu ya haraka ya changamoto na kubadilisha maisha ya mamilioni ya watu duniani, ndiyo kauli mbiu ya Umoja wa Mataifa (UN) inayohimiza kubadilika na kuboresha maisha kwa kutumia ubunifu na ugunduzi.

"Mazoea ya kutekeleza majukumu kwa njia zilizozoeleka hautatusaidia kufikisha kwenye malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) yatupasa kuwa wabunifu, kufikiria ufumbuzi wa changamoto za siku zijazo na kutoogopa kujaribu mambo mapya," anasema Kaimu Mratibu, Mkazi wa UN na Mwakilishi wa Mpango wa Chakula Duniani (WFP) nchini, Michael Dunford.

Anayasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam wakati Ofisi za UN, Mtandao wa Ubunifu wa UN (UNIN) na Kituo cha Ubunifu cha Mpango wa Chakula wa Duniani, walipoandaa usiku wa ubunifu wa mashirika yote ya umoja huo nchini na kuonyesha kazi mbalimbali na jinsi ubunifu ulivyo mwarobaini wa kumaliza changamoto za jamii nyingi nchini.

Dunford anahimiza utamaduni na kujenga mazingira wezeshi ya kuleta ubunifu na kufanya mambo mapya akisema ni muhimu katika kuibua njia mpya za utendaji katika UN .

Ili kufanikisha azma hiyo mashirika mengi ya UN yameunda timu za kuhamasisha ubunifu kidunia na katika mataifa wanapofanyia kazi.

Kwa UN Tanzania harakati za ubunifu zinaendeshwa na Kituo cha Ubunifu cha WFP na Mtandao wa Ubunifu wa UN -UNIN, anasema Dunford na kuongeza: "Kupitia safari ya ubunifu maofisa 30 kutoka mashirika 11 ya UN wamejifunza na kutumia njia mbalimbali za ubunifu zilizoainisha kikamilifu njia bora za kutatua matatizo kama vile, kuibua mbinu za kufanya mawasiliano yenye ufanisi zaidi na wadau na wahisani wa UN.

Je, tutafanya nini ili kupata nishati endelevu kwa ajili ya watu wanaoishi katika kambi za wakimbizi?"



Mwakilishi wa WFP nchini, Michael Dunford, akizungumza wakati wa Siku ya Ubunifu UN. **PICHA: WFP**

**CHANGAMOTO**

Matatizo yanayoikabili dunia pamoja na Tanzania ambayo yanatatuliwa na UN na mashirika yake na yanayohitaji teknolojia na ubunifu ni pamoja na kutoweka kwa kasi kwa maliasili na rasilimali, kwa mfano misitu, ukosefu wa nishati mbadala, mabadiliko ya tabianchi yanayoambatana na mvua kubwa zenye mafuriko, ukame, wadudu waharibifu wa mazao, njaa, mahitaji makubwa ya huduma muhimu za afya, ukosefu wa ajira na kwa ujumla yote hayo yanahitaji ubunifu ili kuyatatua.

**POMBE KUTUMIA KUPIKIA**

Victor Akim, kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), anaelezea kazi ya kibunifu ya kuhamasisha kutumia sukari guru kutengeneza nishati mbadala ya kupikia nyumbani ili kupunguza uharibifu wa misitu inayokatwa kupata kuni na mkaa anataja ubunifu wa kutumia pombe kupikia vyakula nyumbani.

Akimu anasema inakadiriwa kuwa wastani wa hekari 400,000 za misitu hutoweka kila mwaka nchini, hali inayoashiria jangwa kama ukataji miti kwa ajili ya kilimo, kuni na mkaa hautadhibitiwa na kwamba matumizi makubwa ya mkaa yapo Dar es Salaam, ambako asilimia 50 ya matumizi yote ni ndani ya jiji hilo.

Anasema UNIDO imebuni mradi wa kutumia mabaki ya sukari guru (molasesi) kutengeneza pombe aliyoiita 'bioethanol' ambayo inaweza kutumiwa badala ya mkaa na kuni na kwamba majaribio yanaanzia Dar es Salaam maeneo ya Tabata na Ilala kwa kusambaza majiko 110,000 kwa kaya za eneo hilo ili waanze kutumia nishati hiyo kuokoa mkaa.

"Ubunifu na teknolojia hii unalenga kushirikiana na sekta binafsi serikali, sekta binafsi na wazalishaji wa sukari kutumia molasesi kutengeneza bioethanol, nishati mbadala inayoweza kupunguza suala la uharibifu wa misitu.

Lakini siyo sukari guru pekee tunalenga pia kutumia mabibo ya korosho na mabaki ya katani," anaeleza Akim alipowasilisha wazo la ubunifu kutoka UNIDO.

Yohana Joachim, kutoka Mtandao wa Ubunifu wa UN, anasema ubunifu si suala la kukwepa kwani unamhusu kila mmoja kujaribu kufanya kitu kipya kwa gharama nafuu ili kuwezesha kubadilisha maisha ya watu wakiwamo wanawake vijijini.

Anawaeleza washiriki kuwa katika jitihada hizi unahitajika ushirikiano, wabunifu, wananchi wanaohudumiwa na kikubwa kuainisha matatizo ya watu , mfano kupata ufumbuzi wa kupunguza shida ya maji vijijini sehemu ambazo wanawake hutembea kilometa nyingi kwa siku nzima kusaka maji.

Anataja mifano ya kazi za kibunifu na teknolojia kama ugunduzi wa visima vya 'mdundiko' ili kusukuma maji vingine vinavyoendeshwa na nishati upepo yote hayo ni mambo yanayolenga kupunguza changamoto za wananchi kwa kutumia sayansi na ubunifu.

Wabunifu hao wanaowasilisha mawazo yao mbele ya wadau wakiwamo mashirika ya kimataifa, serikali, washirika wa maendeleo na sekta binafsi wanaibua majibu ya maswali mengi yakiwamo jinsi ya kutumia mafuta machafu kutengeneza mvuke nishati utakaotumiwa katika kambi za wakimbizi .

Baadhi ya mashirika ya UN nchini yanayoonyesha kazi mbalimbali za kiubunifu ni pamoja na Shirika la Kilimo na Chakula (FAO) Kazi (ILO) Mazingira (UNEP), Sayansi na Teknolojia (UNESCO) na Wanawake (UN Women).

MAKALA

# Wizara Afya yataja mbinu za kukabiliana na corona

**Na Sabato Kasika**

KATIKA lugha ya Kiswahili, kuna msemo kwamba: "Ukiona mwenzio ananyolewa, wewe tia maji," ukimaanisha kuwa jambo linalomkuta mtu wa karibu yako, basi jiandae kukabiliana nalo.

Msemo huu unaweza kutumika hata kwenye sakata hili linaloendelea la mlipuko wa ugonjwa wa corona ambao umeua zaidi ya watu 100 katika nchi ya China.

Siyo kwamba upo katika nchi za Bara la Asia tu, bali sasa inaelezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba zipo baadhi ya nchi za Afrika ambazo zimetangaza kuwa na watu waliopata maambukizi ya virusi vya corona.

Nchi za Afrika zinazotajwa na shirika hilo ni jirani wa Tanzania ambayo ni Kenya, Zimbabwe, Ivory Coast, Ethiopia na Mauritius.

Kutokana na tishio hilo, serikali imeamua kuchukua hatua za tahadhari kwa wananchi.

Hatua zilizochukuliwa na serikali ni kutenga maeneo matatu maalum kwa ajili ya matibabu kwa washukiwa wa mlipuko wa virusi vya homa hiyo ya mapafu.

Maeneo yaliyotengwa kwa matibabu na kupokea washukiwa wa ugonjwa huo ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, Hospitali ya kudhibiti magonjwa ambukizi ya Buswelu ya Mwanza na Hospitali ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Hiyo ni taarifa ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, iliyotolewa kwa umma juzi.

Waziri anasema, kuna washukiwa walioripotiwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, ambao wamegunduliwa Kenya, Zimbabwe, Ivory Coast, Ethiopia na Mauritius.

"Serikali itatoa taarifa rasmi baada ya uthibitisho kufanyika, ingawa nchini hadi sasa hakuna mgonjwa wala mtu yeyote aliyehisiwa kuwa na ugonjwa huo," anasema Ummy.

Kitendo cha serikali kuchukua hatua hizo ni sawa na kutekeleza wasiwasi ule wa ukimuona mwenzio ananyolewa na wewe tia maji.

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Waziri Ummy anasema, serikali imechukua hatua kadhaa, katika kukabiliana na tishio la ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa wasafiri wote kutoka Bara la Asia.

Anasema, uchunguzi huo unafanyika kwenye mipaka yote ikiwamo viwanja vya ndege vya Mwalimu Julius Nyerere (JNIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Mwanza na Bandari ya Dar es Salaam.

Anasema, kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita, wamefanya uchunguzi kwa raia 1,520 waliingia nchini wakitokea China na Asia kupitia mipakani na viwanja vya ndege. "Ugonjwa huo umekuwa ukisambaa kwa kasi, ambapo kumekuwa na ongezeko la wagonjwa pamoja na vifo, katika kipindi kifupi kwa wastani wa zaidi ya wagonjwa 200 kwa siku," anasema.

Kutokana na hali hiyo, wizara inaendelea kuchukua na kupima sampuli kutoka maeneo ya ufuatiliaji na yeyote atakayehisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo, sampuli zitafikishwa kwenye maabara ya taifa na kupimwa.

Kwamba baada ya hapo, serikali itatoa taarifa rasmi uthibitisho ukishafanyika,lakini hadi sasa hakuna mgonjwa wala mtu yeyote aliyehisiwa kuwa na ugonjwa huo nchini.

**IDADI YA VIPIMO**

Anasema wizara yake ina vipima joto 140, ikiwa vinavyotumia mkono 125 na vile vinavyopima kwa makundi 15, vinatumika katika maeneo mbalimbali ya mipakani ikiwamo viwanja vya ndege na bandari.

Waziri anasema, hadi sasa watumishi wa sekta ya afya 2,297 wameshapatiwa mafunzo ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na majanga ikiwamo jinsi ya kutoa matibabu ya magonjwa ya mlipuko, kuchukua sampuli, uelimishaji na kufuata kanuni za afya.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona na ni kipya 'Novel (New) Corona virus 2019'ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013," anasema.

Inaelezwa kuwa ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja, kukohoa, kupiga chafya au kwa kugusa majimaji ama makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Ummy anataja dalili za ugonjwa huo kuwa huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu mtu kupata maambukizo.


Taarifa rasmi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), zinasema kwamba, tangu mlipuko wa ugonjwa huo uanze katika mji wa Wuhan uliopo Jimbo la Hubei nchini China Desemba 2019 hadi 28 Januari 2020, jumla ya watu 4,593 wamethibitishwa kuugua ugonjwa huo duniani kote.

Aidha, takwimu hizo zinaonyesha kuwa kati ya wagonjwa 4,537, vipo vifo 106 kutoka China, na kwamba ugonjwa huo umeshasambaa, katika mataifa mengine 14 duniani ikiwamo Japan, Jamhuri ya Korea, Vietnam, Singapre, Australia, Malaysia, Cambodia, Thailand, Nepal, Sri Lanka, Marekani, Canada, Ufaransa na Ujerumani.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 30 00)




Dondoo: Kulia

1. Shangwe
8. Samaki kuvutia hewa
9. Mdudu aenezaye Malaria
10.Mjumbe wa Mungu
11.Muasisi wake ni Nkrumah
12.Gurudumu la gari
13.Binadamu
14. Alfabeti ya 19 ya kigiriki
15.Toa mtu usingizini
16.neno la kutilia mkazo
20.Utulivu uliopo mahali
24.Nguo ya Syria
21.Bainika
25.Lokesheni
26.Onyesha uso wa furaha

Dondoo: Chini

1. Kutoweza kufanyika jambo
2. Kumi na nne
3. Jumla ya mali iliyo nayo nchi
4. Gari kubwa la kifahari
5. Sitini na nne
6. Mwanaume kama mwanamke
7. Mnyama mjanja katika ngano
17.Tarakimu
18.Maisha ya raha sana
19.Ukosefu wa maji ardhini
22.Chukua kwa siri
23.Ubinadamu

Jibu toleo lililopita





Waziri Mkuu wa Uingereza, Borris Johnson.

# UINGEREZA NJE YA BREXIT

## ■Tamu, chungu watakayokutana nayo

**Na Mwandishi wetu**

USIKU wa kuamkia leo, Uingereza imejitoa rasmi katika Muungano wa Ulaya (EU) na kuwa nchi pekee inayojitegemea katika bara hilo lenye nguvu za kiuchumi.

Mpaka inatimiza ndoto hiyo ambayo ilipigiwa kura na idadi kubwa ya Waingereza, ndani ya miaka mitatu mawaziri wa wakuu watatu walikabiliana na joto kali mchakato huo kujiondoa, hatimaye waliamua kujiuzulu.

Waziri Mkuu wa sasa Boris Johnson, alikabiliana na vikwazo ambavyo wenzake walipitia na kushindwa, lakini yeye alifaulu na nchi hiyo sasa imeondoka rasmi.

Pamoja na furaha ya Waingereza wengi kuona wanaondoka katika muungano huo, lakini watakabiliana na kipindi cha mpito cha miezi 11 kabla ya kujitegemea.

Nini kitabadilika?

Kwa mujibu wa Shirika la BBC, wakati wa kipindi cha mpito Uingereza itaendelea kufuata sheria za EU na kutoa mchango wake wa kifedha.

Wabunge wa Uingereza kupoteza viti vyao

Nigel Farage, kiongozi wa chama cha Brexit na mwanaharakati anayeunga mkono kampeni ya Uingereza kujiondoa katika Muungano wa Ulaya, atakuwa mmoja wa wabunge 73 wa Uingereza katika bunge la Ulaya watakaopoteza viti vyao.

Hii ni kwa sababu Brexit ikifanyika Uingereza italazimika kujiondoa katika taasisi za kisiasa za EU na mashirika yake.

Uingereza itafuta sheria ya Uingereza katika kipindi cha mpito, Mahakama ya Haki ya Ulaya itaamua jinsi sheria za EU zitakavyotekelezwa.

**HAIRUHUSI MIKUTANO EU**

Waziri Mkuu wa Ungereza, Boris Johnson, atapewa mwaliko maalum endapo atataka kuungana na viongozi wengine katika kongamano la baraza la Ulaya siku zijazo.

Mawaziri wa Uingereza pia hawatahudhuria mikutano ya mara kwa mara ya muungano huo ambayo inaamua masuala kadhaa muhimu.

**MASUALA YA KIBIASHARA**

Uingereza itaweza kuanza mazungumzo ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani kuhusu kuweka taratibu mpya wa kununua na kuuza bidhaa na huduma.

Haikuruhusiwa kufanya mazungumzo na nchi kama Marekani na Australia wakati ikiwa mwanachama wa Umoja wa Ulaya. Kambi inayounga mkono kujitoa kwa Uingereza inasema kuwa itakuwa na uhuru wa kuweka sera zake za kibiashara kwa ajili ya kuinua uchumi wake.

Kuna umuhimu wa kujadiliana na EU kuhusu kukubaliana kibiashara kati ya Uingereza na EU.

Ikiwa itafikia makubaliano ya kibiashara, hawataweza kuanza mpaka kipindi cha mpito kitakapokamilika.

**PASIPOTI ITABADILISHWA RANGI**

Akitangaza mabadiliko hayo mwaka 2017, Waziri wa Uhamiaji, Brandon Lewis, alisifia kurejea kwa pasipoti ya kipekee za rangi ya bluu na dhahabu, ambazo zilitumika mwaka 1921.

**SARAFU YA BREXIT**

Karibu sarafu milioni 50 zilizo na alama ya tarehe "Januari 31" na iliyoandikwa: "Amani, mafanikio, urafiki na mataifa yote", itaanza kutumika Ijumaa.

Sarafu hizo zimepokelewa kwa hisia mseto, huku wafuasi wanaotaka kubaki wakisema hawaikubali.

Serikali ilikuwa imepanga kuzindua sarafu hiyo Oktoba 31, tarehe ya awali iliyowekwa kwa ajitoa Brexit.

Hata hivyo sarafu hizo ziliyeyushwa na kuundwa tena baada ya muda wa mwisho kurefushwa.

**IDARA BREXIT KUFUNGWA**

Jopo la mashauriano ya Uingereza na EU limekuwa likiongoza mchakato wa Brexit litavunjwa. Idara inayoendesha mchakato wa Uingereza kujiondoa Muungano wa Ulaya iliundwa na waziri mkuu wa zamani wa Uingereza Theresa May, mwaka 2016.

Kwa mazungumzo yatayofuata, timu ya mashauriano ya Uingereza itakuwa na makao yake Downing Street.

**UJERUMANI HAITABADILISHA-NA WAFUNGWA NA UINGEREZA**

Haitawezekana kuwarejesha Uingereza watu wanaoshukiwa kuwa wahalifu waliotorokea Ujerumani. Katiba ya Ujerumani hairuhusu raia wake kushtakiwa katika nchini nyingine isipokuwa mataifa ya Muungano wa EU.

"Hatua hii haiwezi kufanyika tena baada ya Uingereza kujiondoa katika Muungano wa EU," Msemaji wa Wizara ya Haki ya Ujerumani aliambia BBC. Haijabainika kama udhibiti huo utahusisha nchi zingine za muungano huo, Slovenia, kwa mfano, inasema hali hiyo ni ya kuchanganya, lakini Tume ya Ulaya haikuweza kutoa tamko lolote kuhusu suala hilo.

Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Uingereza inasema waranti ya kukamatwa ya Ulaya itaendelea kuzingatiwa katika kipindi cha mpito.

**MAMBO HAYATOBADILIKA**

Katika kipindi cha mpito vitu vingi vitasalia kama kawaida hadi tarehe 31 mwezi Desemba 2020:

Usafiri wa ndege, boti na treni zitaendelea kuhudumu kama kawaida. Linapokuja suala la udhibiti wa pasipoti, katika kipindi cha mpito, raia wa Uingereza wataruhusiwa kupanga foleni katika eneo lililotengewa raia wa mataifa ya EU.

Leseni halali zitaendelea kutumika na kadi za bima zinazotolewa na serikali kwa raia wa Uingereza ili wapate huduma za matibabu wakiwa wagonjwa au wakipata ajali. Uhuru wa kusafiri utaendelea kuzingatiwa katika kipindi cha mpito, kwa hivyo raia wa Uingereza wataweza kuishi nchini humo na kufanya kazi nchi yoyote ya EU kama wanavyofanya sasa.

Raia wa Uingereza wanaoishi katika mataifa wanachama wa Muungano wa Ulaya wataendelea kupokea malipo yao ya uzeeni na pia nyongeza yao ya kila mwaka.

Pia Uingereza itaendelea kuchangia bajeti ya EU wakati wa kipindi cha mpito, itaendelea kufadhiliwa.

Biashara kati ya Uingereza na Muungano wa Ulaya itaendelea bila malipo yoyote ya ziada au kubuniwa kwa sheria mpya za forodha.

## HABARI KIMATAIFA

# Uingereza yatangaza kuingia corona

**LONDON, Uingereza**

WATU wawili wamegundulika kuwa na virusi vya corona nchini Uingereza, mkuu wa idara ya afya nchini humo ametangaza.

Katika taarifa hiyo, inasema watu wote wanatoka katika familia moja na sasa wanapata matibabu.

Hakuna taarifa iliyotolewa zaidi kuhusu familia hiyo na wapi wanapopatiwa matibabu.

Takriban watu 213 nchini China wamepoteza maisha kutokana na virusi hivyo, hasa kutoka mjini Hubei, huku kukielezwa kuwa na watu 10,000 wameathirika nchi nzima.

Watu 98 wamegundulika kuwa na virusi katika nchi nyingine 18.

Shirika la Afya Duniani limetangaza mlipuko wa virusi vya corona ni janga duniani.

Kwa sasa, raia 83 wa Uingereza na 27 wa mataifa ya kigeni wanarejea Uingereza kutokea Wuhan, mji ambao ni kitovu cha mlipuko nchini China.

Abiria hao watawekwa karantini katika Hospitali ya Arrowe Park kwa majuma mawili.

Profesa Chris Whitty, ofisa mkuu wa matibabu nchini England alisema: Idara ya afya nchini Uingereza imejiandaa vya kutosha na ina uzoefu wa kuzuia maambukizo na tayari tunafanya kazi mara kwa mara kutambua wale waliokaribiwa na wagonjwa ili kuzuia maambukizo zaidi.

Tumejiandaa kuzuia vifo vya ugonjwa huo, Uingereza na virusi vya corona na tuna njia nyingi za dharura kukabiliana na virusi hivyo, aliongezea.

Profesa Whitty alisema kwamba Uingereza inafanya kazi kwa karibu na Shirika la Afya Duniani WHO pamoja na jamii ya kimataifa huku mlipuko huo nchini China ukiendelea ili kuhakikisha wako tayari kwa lolote litakalotokea.

WHO lilitangaza Alhamisi.

Idadi ya vifo vya virusi vya corona duniani sasa imepita mlipuko wa virusi vya SARS, ambayo vilisambaa kwa zaidi ya mataifa 18 mwaka 2003.

Kufikia sasa raia 83 wa Uingereza na wengine 27 raia wa kigeni wanasafiri kurudi nchini Uingereza kutoka Wuhan, mji wa China ambao ndio chanzo cha mlipuko huo.

Ndege hiyo inatarajiwa kutua katika kambi ya wanahewa ya RAF Brize Norton.

Abiria wa Uingereza baadaye watapelekwa hadi Hospitali ya Arrowe Park na kutengwa kwa wiki mbili.

*BBC*



Wafanyakazi wa Shirika la Ndege la Skoti wakiwasili Singapore kutoka Wuhan China ambako kuna mlipuko wa virusi vya corona. Abiria wa ndege hiyo N95 walivaa vitambaa maalum vya puani kujikinga na ugonjwa huo. **(PICHA: AFP)**

## Bilionea afuta ombi mwanamke kwenda naye mwezini

**TOKYO, Japan**

TAJIRI ambaye pia ni mwanamitindo maarufu amefuta ombi lake la kumtafuta mwanamke atakayekwenda naye katika ziara ya mwezini.

Katika mwaliko huo aliwataka wanawake wenye umri chini ya miaka 20 na ambao hawajaolewa wawasilishe maombi yao kwa ajili ya safari hiyo ya kipekee ya kimahaba.

Karibu wanawake 28,000 walituma maombi, lakini Alhamisi alisema kuwa amepatwa na hisia tofauti kuhusu suala hilo na ameamua kufutilia mbali wazo hilo.

Bado ana mpango wa kuendelea na ziara yake mwezini mwaka 2023 bila mpenzi.

Mapema mwezi Januari, bilionea huyo wa miaka 44 alitoa tangazo mtandaoni kumtafuta mpenzi wa kike atakayeandamana naye mwezini.

Tovuti yake ilikuwa imeweka masharti pamoja na maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha maombi katika mchakato huo uliochukua miezi mitatu.

Katika ombi la mtandaoni, Maezawa anasema kuwa anataka kufurahia safari hiyo na mwanamke wa kipekee.

Masharti ya kushiriki lazima uwe bila mpenzi, uwe na miaka zaidi ya 20, uwe na mtazamo mzuri wa maisha na ufurahie kuzuru anga za mbali.

Muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi ni Januari 17, ambapo uamuzi wa mwisho kuhusu mpenzi wa Maezawa ulikuwa utatolewe mwisho wa mwezi Machi.

Lakini Alhamisi, aliweka tangazo katika Twitter akisema kuwa hana haja tena ya kutafuta mpenzi wa kwenda nae mwezini.

**BBC**

# Marekani yadai corona itainufaisha kiuchumi

**WASHINGTON, Marekani**

KATIBU wa Rais Donald Tramp, katika masuala ya biashara, Wilbur Ross, amesema mlipuko wa virusi vya corona nchini China unaweza kuinua uchumi wa Marekani.

Wakati wa mahojiano katika runinga moja, Ross alisema anadhani virusi hivyo vitasaidia kurudisha ajira kaskazini mwa Marekani.

Kuenea kwa kasi kwa ugonjwa huo kumezua hofu kuhusu athari zake katika uchumi wa China na ukuaji wa uchumi kwa jumla.

Matamshi hayo yamepokewa kwa hisia kali kutoka kwa wakosoaji wa utawala wa Rais Trump.

Akijibu swali kutoka kwa mwandishi wa Fox kuhusu iwapo mlipuko huo ni hatari kwa uchumi wa Marekani, Ross alisema, "Sitaki kuzungumzia kuhusu mafanikio kuhusu ugonjwa huu hatari. Ukweli ni kwamba unatoa fursa kwa biashara. Hivyo basi nadhani utasaidia kuongeza ajira kaskazini mwa Marekani," aliendelea kusema.

Baadaye Wizara ya Biashara iliunga mkono matamshi yake: "Kama katibu Ross alivyoweka wazi kitu cha kwanza ni kuhakikisha kuwa virusi hivyo vinadhibitiwa na baadaye kuwasaidia waathiriwa wa ugonjwa huo. Pia ni vyema kutazama athari za kufanya biashara na taifa ambalo lina historia ya kuzuia hatari nyingi kwa watu wake na dunia nzima kwa jumla," alisema msemaji.

Matamshi hayo yamekosolewa na Mbunge wa Chama cha Democrat, Don Beyer, ambaye katika ujumbe wake wa Twitter aliuliza vipi mtu anaweza kuchukua fursa ya kibiashara katika mlipuko mkubwa.

Wanauchumi pia wameuliza maswali mengi kuhusu matamshi ya Ross, akiwamo Simon Baptist kutoka kitengo cha ujasusi cha Singapore aliambia BBC kwamba matamshi hayo yalimshangaza yeye binafsi.

"Kampuni hazitaweza kupata uwekezaji wa kipindi kirefu kutokana na mlipuko ambao huenda ukaathiri watu kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita," alisema.

Alisema kwamba virusi hivyo huenda vikawa na athari mbaya badala ya nzuri.

"Ukweli ni kwamba Marekani itapoteza kwa sababu licha ya kila kitu China ni soko lake kubwa, hivyo basi iwapo uchumi wa China utapunguza kasi katika ukuaji wake utaathiri uchumi wa Marekani vilevile".

Takriban watu 213 wamefariki kutokana na virusi hivyo nchini China na sasa vimesambaa hadi katika mataifa 18 mengine.

Wanauchumi wamesema kwamba virusi hivyo vya corona vinaweza kuwa na athari kubwa katika uchumi zaidi ya virusi vya Sars vilivyozuka kati ya 2002-2003.

Sars uliambukiza watu 8,000 na kusababisha vifo vya watu 700 na unakadiriwa kugharimu uchumi duniani takriban dola bilioni 30.

Virusi vya corona vimelazimu kampuni mbalimbali duniani zikiwamo zile za teknolojia, watengenezaji magari na wauzaji kufunga kwa muda nchini China huku mamlaka ikiendeleza likizo ya kusherehekea mwaka mpya na kuweka vikwazo vya usafiri katika taifa hilo.

*BBC*

# HADITHI

# Jumba Jekundu-38

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

Eliza aliyekuwa amekaa sambamba na Edina, pamoja na urembo alionao, lakini alikiri moyoni kuwa amekutana na kiboko yake.

Pamoja na hayo, aliona kabisa kuwa moyo na akili za Kadili siku zote zilikuwa kwa Edina na si yeye.

Ni kweli alikubali kuolewa na Kadili kama dili lilivyopangwa na baba yake mzazi na dada yake ambaye ni mama Kadili ili waoane mtu na dada yake binamu, lakini tangu afike pale, aliona dalili zote za Kadili kuwa haziko kwake, bali kwa binti huyo ambaye leo ndiyo amemuona kwa macho yake.

Kwa mbali furaha ilimjia kwani sasa atakuwa huru kuchagua mtu ampendaye na si kulazimishwa tena na familia kama ilivyotaka iwe.

Mgeni aliaga. Mama alimkumbatia mkwewe mtarajiwa. Machozi yaliwatoka.

“Sasa mama mimi hapa ni mwenyeji, hapa ni nyumbani kwangu.” Edina alimwambia Mama Kadili.

“Karibu mwanangu.”

Safari hiyo ilitoka hapo na kwenda kwa kina Meze. Edina alitaka ajue sehemu zote ambazo rafiki zake aliokuwa akikutana nao disco miaka kadhaa iliyopita.

Awali safari ilikuwa ni wa watu watatu, Kadili, Edina na Meze. Lakini safari hii aliongezeka mmoja.

Meze ambaye alirejea baadaye kungana na familia ya rafiki yake kula chakula cha mchana, alikuwa anatoka hapo na rafiki zake hao wawili, lakini akiongezeka Eliza.

Huko hakukaa sana na tayari giza lilikuwa limeshaingia, hivyo wenyeji wake watatu walimpeleka alipopaki gari lake.

“Kadili, Meze na shoga’angu Eliza, wiki ijayo nitakuwa na pati kubwa nyumbani linalohusu tukio hili lililotokea leo la kihistoria. Nitawaandalia sherehe fupi hivi, kwa hiyo mjiandae nakuja kuwachukua mimi mwenyewe.” Alisema Edina na kuongeza.

“Hii pati mama haimhusu, itakuwa ni ya vijana tu kwa sasa sisi wenyewe, yeye mama nitakuja kumchukua siku nyingine aende akapajue nyumbani.”

“Asante wifi yangu, wala usikonde.” Alijibu Eliza.

Alipofungua mlango, kabla ya kuingia, alimtazama Kadili na kumkumbatia.

Wakati wakiwa na bahari ya mahaba, Kadili aligeuza kichwa nyuma yake.

Macho yake yaliwaona Meze na Eliza wakiwa wanawaangalia kwa tabasamu, halafu na wao wanatazama usoni.

***************************




Siku tatu baadaye, Kadili na rafiki yake Meze walikutana kwenye kijiwe chao. Kwenye mkungu ulio mita chache kutoka kwenye duka na nyumba ya mjomba wake Meze.

Kadili alishaona yake yanamuishia. Baada ya tabu zote, anakwenda kuwa mume wa msichana tajiri.

Lakini safari yake yote na tabu zote kulikuwa na watu waliokuwa nyuma yake, wakisaidia kwa ushauri, hali na hata kisaikolojia hadi kufika hapo alipofikia.

Wa kwanza alikuwa rafiki yake mkubwa Meze. Tangu siku ya kwanza walipokutana na Edina wakiwa disco alikuwa naye.

Ushauri na matatizo yote wapo wote, hadi kufikia pale alipofika, hakuna hata kimoja ambacho hajawahi kumhadithia rafiki yake, naye pia kutoa ushauri wake.

Mwingine ni Eliza. Binamu yake. Mtoto wa mjomba wake ambaye alichukuliwa kutoka Mtoni Mtongani na kuletwa Tandale kwa ajili ya kumtuliza na hatimaye mbele ya safari afunge naye ndoa kwa sababu ya kumuondoa kwenye mawazo ya msichana Edina ambaye awali ilionekana ni ngumu kwake kumpata kutokana na mazingira magumu ya wakati huo. Lakini sasa mambo yalikuwa shwari na Eliza ni kama siku zake za kuishi nyumbani kwao zinamalizika.

Alijiona ni kama mwenye hatia kumweka mtu miezi mingi, akiishi hapo, halafu hakuna kitu kilichoendelea zaidi ya kumrudishwa kwao Mtoni Mtongani, huku akiwa amepotezewa muda.

“Meze kuna kitu nataka kukwambia naomba unisaidie.” Kadili alimshtua rafiki yake.

“Jambo gani tena hilo mwanangu, mbona tunaanza kushtuana tena.”

“Hapana si baya, ila halitakuwa baya kama utanipa msaada wako.”

“He, Kadili siku hizi, tangu demu wa kishua kakukubali umekuwa na maneno kweli.”

“Hapana, nina jambo muhimu kweli.”

“Haya hebu niambie.” Meze alikaa tayari kusikiliza.

“Unamchukuliaje Eliza?”

“Eliza si kama dada yangu na upande shemeji yangu.”

“Shemeji yako kwa nani?” Kadili alijibu huku akitabasamu.

“Si wewe ulitaka kumuoa?” Meze alijibu akimtazama Kadili kwa makini usoni.

“Sasa sitomuoa tena, unajua hilo?”

“Najua.”

“Sasa nataka unisaidie wewe.” Kadili alisema, lakini Meze alionekana bado hajamwelewa.

“Eliza ni msichana mzuri au si mzuri?” Kadli aliongeza swali kabla hata Meze hajajibu.

“Ni msichana mzuri sana.”

“Sasa mimi ni kaka yake binamu, na wewe ni rafiki yangu, naomba umuoe Eliza.”

> **“Kama muoaji yupo na muolewaji yupo, mengine niachie mimi, ninachotaka ukubali, ila kama umempenda.” “Hakuna mwanaume yoyote anayeweza kumkataa Eliza, ila yeye atakubali kweli na wazazi wake, hasa mama yako atakubali?”**

Maneno hayo yalimshangaza sana Meze. Alibaki kimya asiamini kinachozungumzwa.

Mawazo yakamrudisha nyuma siku Eliza alipokwenda dukani kwake kununua mafuta ya kupikia chapati, lakini pia kumuulizia Kadili ambaye hakuonekana nyumbani kutwa nzima. Akayakumbuka mazungumzo waliyokuwa wakizungumza.

“Eliza wacha wivu, mumeo mtarajiwa atarudi tu, au unadhani yuko na wanawake wengine?’ Alihoji. “Mhh, hapana usalama wake muhimu kwanza.”

“Siyo wivu bibie?”

“Hapana sina wivu kwa sababu sidhani kama rafiki yako ananipenda hasa.”

“Kwa nini?”

“Huo unafiki, hata wewe unajua hilo. Kuna mtu anampenda, ndiyo anayemsumbua, na mimi nimekuwa kama mbadala tu, ikishindikana kabisa ndiyo anioe mimi.”

“Sasa hilo linakukwaza?”

“Sana tu, nimekubali kwa sababu wanaotaka hili litimie ni shangazi yangu, mama yake Kadili na baba yangu mzazi mzee Tengeneza, kaka yake shangazi, vinginenvyo nisingekubali.”

“Ila kuolewa unataka?”

“Meze, hakuna mwanamke asiyekubali kuolewa. Lakini anataka kuolewa na mwanaume anayempenda na kumjali, lakini kwangu mimi kwa Kadili ni kama spea tairi ambalo linasubiri lingine liharibike, ndiyo litumike, kama halikuharibika ndiyo basi tena.”

“Kama mimi nigekuwa Kadili, saa hizi ningekuwa nimeshakuoa.” Maneno hayo yalimtoka Meze bila kutarajia.

“Inawezekana wewe unajua thamani yangu na si rafiki yako.”

“Hakika, Eliza wewe ni mwanamke mrembo, mwenye kila sifa ya kuwa malkia ndani ya nyumba. Bahati hii haikunikuta mimi, nisingeipoteza.”

“Haijakukuta kwa sasa, lakini huenda baadaye ikakukuta.” Alijibu.

“Nadhani sasa ndiyo hii inataka kunikuta.” Alijisemea mwenyewe baada ya kutoka kwenye lindi la mawazo akiwaza siku ile walipokutana na ndiyo siku ambayo mama Gombea akaenda kumshtaki kwa mama Kadili kuwa Meze anamzunguka rafiki yake kwani aliwakuta laivu wakitongozana.

Anakumbuka alimwambia kama ingekuwa yeye angeweza kumuoa. Na Eliza hakuonekana kupinga.

“Nadhani umenisikia, lakini bado hujanijibu Meze.” Kadili alimshtua rafiki yake.

“Ni kweli Kadili, mimi sina mpenzi, umri wa kuona tayari, lakini haya ni mambo ya kujipanga.”

“Kama muoaji yupo na muolewaji yupo, mengine niachie mimi, ninachotaka ukubali, ila kama umempenda.” “Hakuna mwanaume yoyote anayeweza kumkataa Eliza, ila yeye atakubali kweli na wazazi wake, hasa mama yako atakubali?”

“Hilo pia niachie mimi.”

“Basi akikubali mimi sina tatizo.” Meze alithibitisha kuwa anaweza kumuoa Eliza.”

Marafiki hao waligongeana mikono. Ghafla moyo wa Meze ulifarijika, kwani alikuwa anampenda Eliza kutokana na urembo, umbile na hata tabia yake ya upole, lakini alikuwa akifungwa na kuwa alitakiwa kuwa mke wa rafiki yake Kadili baadaye, lakini mambo yamebadilika na sasa Kadili mpango wake wa kuoana na Edina unaonekana kukamilika.

*Itaendelea Jumamosi*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**

Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji

**Apige: SImu Namba:**

**0786 641903 au 0716 172929**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**Geofrey Juma** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0344/026 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 1991 katika Shule ya Sekondari Shirati.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: TAR/RB/81/07

215612002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No;10/2020**
Ombi la MARY COSTA MBENA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PROSPER ILDEFONS FUIME.** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/01/2020.

215612102


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose*

*Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0782253676*



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MESSI
## AFIKISHA MECHI 500 ZA USHINDI BARCA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi ameweka rekodi nyingine na Barcelona, akiwa sasa amecheza mechi 500 za ushindi kwa klabu hiyo.

Messi alifunga mara mbili na kuchangia mengine matatu wakati Barca ikiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Leganes kwenye mchezo wa Copa del Rey, Alhamisi.

Hiyo imemfanya Messi kuwa mchezaji wa kwanza kufikia rekodi hiyo katika klabu hiyo, Xavi akishinda mechi 476 na Andres Iniesta akifikisha mechi 459 hapo kwenye dimba la Camp Nou.

Espanyol ilikuwa timu ya kwanza kufungwa na Barca iliyokuwa na Messi ndani Oktoba mwaka 2004.

Wakati huo huo, UDA Gramenet ndio timu pekee iliyocheza Messi akiwa ndani na kuepuka kipigo, ikiwa imeifunga Barca kwenye Copa del Rey msimu wa 2004-05.

Kwa ujumla wa Messi amekuwa kwenye kikosi cha ushindi dhidi ya timu tofauti 86, huku Sevilla ndio timu aliyoionea zaidi.

Messi ameshinda mara 29 dhidi ya klabu hiyo ya Andalusia, huku akishinda mara 24 dhidi ya Atletico Madrid na mara 19 dhidi ya Real Madrid.

# ROJO AREJEA ARGENTINA


**BOANES ARIES, Argentina**

BEKI wa Manchester United, Marcos Rojo amerudi katika klabu ya Argentina ya Estudiantes kwa mkopo wa muda mfupi.

Rojo, ambaye alikuwa anakaribia kujiunga na Everton, amekuwa na wakati mgumu wa kupata namba kwenye kikosi cha United msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alisajiliwa kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 16 kutoka Sporting CP mwaka 2014, na sasa ameondoka Old Trafford, akirudi Estudiantes - ambako alianzia kucheza soka kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu.

Akiwa na uwezo wa kucheza beki ya kati au kushoto, Rojo amekuwa akisumbuliwa na majeruhi wakati wake hapo United na amecheza mechi 76 za Ligi Kuu England kwa ujumla.



Estudiantes, ambao wapo nafasi ya 12 kwenye Ligi Kuu Argentina, Superliga, walikuwa wa kwanza kutangaza dili hilo, wakiweka video kwenye ukurasa wao wa Twitter pamoja na maneno yasemayo: "Mara zote umerudi kwenye sehemu ambayo unakuwa na furaha.

"Ndoto yako ya kuwa tena na familia hii imetimia. Tumekutana tena. Karibu na asante kwa kuja tena Marcos. Karibu na moyo wako wote."

Awali Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alibainisha kwamba hatarajii kuona Rojo akiondoka wakati wa dirisha hili dogo la usajili la Januari.

# Coman arudi mazoezini Bayern

**MUNICH, Ujerumani**

MCHEZAJI Kingsley Coman amerudi kwenye mazoezi katika kikosi cha Bayern Munich Alhamisi wakati akiendelea kupona majeruhi yake ya goti.

Coman amekuwa nje ya dimba tangu alipoumia goti lake la mguu wa kushoto wakati wa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Tottenham Desemba mwaka jana.

Hata hivyo, awali alirudi uwanjani, lakini hakuwa fiti na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa sasa amejiunga na wachezaji wenzake wa kikosi cha kwanza.

Bayern ilithibitisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amefunga mabao manne kwenye mashindano yote msimu huu, alimaliza dakika 45 za mazoezi, akipiga mashuti kabla ya kupewa nafasi ya kujifua peke yake.

Klabu hiyo imebainisha kuwa ni Niklas Sule pekee ambaye bado anajiuguza ndiye aliyekosa mazoezi hayo, huku Javi Martinez akianza kufanya mazoezi ya peke yake.

Kikosi hicho cha kocha, Hansi Flick kipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kikipitwa pointi moja na vinara RB Leipzig.



## HABARI MICHEZO

# MATIC

## ATAKA MKATABA MPYA UNITED

**MANCHESTER, England**

NEMANJA Matic amesema anataka kubakia Manchester United na atakataa ofa yoyote kutoka klabu nyingine kama atapewa ofa ya kuongeza mkataba wake.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Serbia, Matic anaweza kuondoka pale Old Trafford akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu kama United haitaamua kumpatia mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameanza katika mechi zote sita zilizopita kwenye mashindano yote na alifunga bao pekee kwenye nusu fainali ya pili ya Kombe la EFL Jumatano dhidi ya Manchester City, kabla ya kutolewa nje kwa kuonyeshwa kadi mbili za njano.

Pep Guardiola alimtaja Matic "mwenye kipaji bora" baada ya mchezo huo na kusema mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea anaweza kupewa mkataba mpya.

"Nina mkataba hadi mwishoni mwa msimu," alisema Matic akiwaambia waandishi wa habari. "Nipo Carrington kila siku na naweza kuzungumza nao kama wanafikiri naweza kuwasaidia. Kama sio, maisha yataendelea.

"Bado hakuna majadiliano yoyote yaliyofanyika, lakini nafasi yangu ipo wazi. Nia yangu ni kuiwakilisha klabu hii. Nimekuja hapa kushinda na kama wanataka mimi nibaki bila shaka nitajitolea kwa hali na mali kushinda mataji.

"Siwezi kusema klabu gani imenifuata hadi sasa, ukiwa unaichezea Manchester United, klabu nyingine zinatafuta kukusajili," amesema.

## NEWCASTLE YAMSAJILI DANNY ROSE

**NEWCASTLE, England**

KLABU ya Newcastle United imemsajili beki wa kushoto wa Tottenham, Danny Rose kwa mkopo hadi mwisho wa msimu.

Rose, ambaye alijiunga na Tottenham mwaka 2007, amekuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa Januari hii na Newcastle, baada ya kuwaongeza wawili kwa mkopo Nabil Bentaleb, mchezaji mwenzake pale Spurs na winga wa Inter Milan, Valentino Lazaro.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 29 ametua hapo kwa ajili ya kuimarisha safu ya ulinzi ya Newcastle baada ya Paul Dummett na Jetro Willems kuwa majeruhi.

Rose, ambaye amecheza zaidi ya mechi 150 za Ligi Kuu kwa Spurs, ameanza mara moja tu tangu Oktoba mwaka jana katika kipigo cha 1-0 kutoka kwa Liverpool Januari 11 mwaka huu.

"Ni heshima kubwa kwangu kuwa hapa. Nina furaha kubwa kuja hapa na natarajia kulipa fadhila kadiri nitakavyoweza haraka inavyowezekana," amesema Rose akiambia NUFC TV.

"Kwa upande wangu, kwa hakika ni jambo la kuvutia kwamba nimekuja hapa na kuwa na nafasi ya kucheza mbele ya mashabiki wa Newcastle.

"Newcastle ni moja ya klabu kubwa England. Nimezungumza na kocha usiku uliopita na aliniambia kuna mashabiki 50,000."



## Lopetegui awaomba radhi Sevilla

**MADRID, Hispania**

JULEN Lopetegui ameomba radhi kwa mashabiki wa Sevilla baada ya timu hiyo kutolewa katika michuano ya Copa del Rey na timu ya Mirandes, Alhamisi.

Sevilla walichapwa mabao 3-1 kwenye mchezo huo wa kufuzu hatua ya 16, huku Matheus Aias akiipeleka Mirandes kipindi cha pili kwa uongozi wa mabao mawili.

"Tunaomba radhi. Wote tunahuzunika, lakini tunatakiwa kurudi kwenye hali yetu haraka," alisema Lopetegui.

"Tulikuwa wafungwa kwa kuanza kwetu vibaya na wakatumia nafasi hiyo kupata mabao ya kuongoza. Katika mfumo huu, mchezo mmoja mbaya maana yake unakuondoa kwenye michuano.

"Bao la kwanza lilikuwa ufunguo wao. Liliwapa nguvu kubwa na bila shaka wakaendelea kutuadhibu.

"Kama ukifanya mabadiliko matatu kwenye mchezo, ni kwa sababu kosa la kwanza lilikuwa la kocha.

"Tulijaribu kufunga mwanzoni mwa kipindi cha kwanza, lakini hatukuweza kila kitu kilikuwa dhidi yetu. Goli tulilolitarajia kuja halikuwezekana, hivyo tukamaliza mchezo kwa kipigo."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# CITY YAJITOKEZA KUMWANIA COUTO

**Yawasilisha ofa kubwa zaidi ya iliyotolewa na Barcelona na Arsenal ili kupata saini ya beki huyo chipukizi ...**

**MANCHESTER, England**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City imeingia katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya beki chipukizi na mwenye thamani ya juu wa Timu ya Taifa ya Brazil, Yan Couto.

Kwa mujibu wa gazeti la Globoesporte la nchini Brazil, limeandika City imejiimarisha kuipiku Barcelona na Arsenal katika kunasa saini ya beki huyo mwenye umri wa miaka 17.

City inaonekana kupata nafasi ya kumsajili beki huyo kwa kuangalia mchakato wa kumpata beki huyo ambaye dau lake linatajwa kuwa ni kati ya pauni milioni 4 na 5, lakini taarifa zinasema City imewasilisha ofa ya juu ya pauni milioni 7.5, ambayo baadaye itapanda na kufikia pauni milioni 12.5.

Couto ambaye anaichezea klabu ya Cortiba ya Brazil hatarajiwi kuondoka kwenda katika timu nyingine yoyote ya Ulaya mpaka kipindi cha majira ya joto kitakapoingia, ambapo Juni mwaka huu atakuwa ametimiza umri wa miaka 18.

Lakini amekanusha tetesi kuwa anaondoka klabuni hapo baada ya juzi Alhamisi kuweka alama ya picha ya ndege katika akaunti yake ya Twitter akimaanisha anasafiri kuelekea katika klabu nyingine.

Picha hiyo ilionekana kuzusha mijadala mbalimbali ambayo mashabiki wake waliamini ameweka ujumbe wa kuwaaga na anaelekea katika maisha mapya.

Lakini tayari beki huyo ambaye amekulia kwenye mfumo wa timu za vijana za Brazil amebainishwa kuwa ni nyota ambaye ana uwezo mkubwa huku mapema mwezi uliopita Arsenal iliweka wazi inataka kumsajili kwa kumpa mkataba wa muda mrefu.

Arsenal iliweka wazi kwamba inamhitaji beki huyo katika kikosi chake ili kurithi mikoba ya Hector Bellerin.

Couto alianza kung'ara akiwa kwenye kikosi cha Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 katika Fainali za Kombe la Dunia za U-17 mwaka jana na kuiongoza Brazil kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwenye ardhi ya nyumbani.

Baada ya mapema Januari mwaka huu Barcelona kuonyesha nia ya kumsajili Couto, Sport ilimtaka beki huyo kuwa ni 'Dani Alves mpya' kwa kumfananisha na beki huyo wa kulia mkongwe.

Klabu ya Bayer Leverkusen ya Ujerumani pia inatajwa kumwania chipukizi huyo.

## KWA UFUPI

**GIROUD ANUKIA LAZIO**

LAZIO imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(Sky Sports)***

**MERTENS ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA ilitarajia kuwasilisha tena ofa katika dakika za lala salama ya kumwania mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Dries Mertens (32), baada ya ofa yake ya kwanza kukataliwa. ***(Telegraph)***

**CAVANI AZIDI KUGOMBEWA**

CHELSEA imejitosa kuwania saini ya straika wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, ambaye mchakato wake wa kujiunga na Atletico Madrid kushindikana. ***(Star)***

**BRUNO AMTOA POGBA**

MANCHESTER United sasa itamruhusu kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba (26), kuondoka katika klabu hiyo kwenye majira ya joto kufuatia kutua kwa nyota wa Ureno, Bruno Fernandes, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sun)***

**MATIC ABAKIA UNITED**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Serbia, Nemanja Matic (31), amekataa ofa ya kuondoka Manchester United na ameweka wazi yuko tayari kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya Old Trafford. ***(Telegraph)***

**JOSE AKARIBIA UNITED**

MABOSI wa Manchester United imempa ofa ya kumsajili straika Mbrazili Willian Jose (28), kwa mkopo akitokea Real Sociedad. ***(Sky Sports)***

**UNITED YAMWANIA RONDON**

STRAIKA wa zamani wa West Brom na Newcastle, Salomon Rondon anatajwa kutakiwa na Manchester United. Nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Venezuela mwenye umri wa miaka 30 kwa sasa anaichezea klabu ya Dalian Yifang inayoshiriki Ligi Kuu China. ***(Times)***

**UNITED YAMKOSA KING**

MANCHESTER United imeshindwa kukamilisha usajili wa mshambuliaji wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Norway, Joshua King, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Telegraph)***

**AUBAMEYANG AITAKA BARCA**

STRAIKA wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye ana umri wa miaka 30, amesema anataka kuondoka The Gunners na kujiunga na Barcelona. ***(Le10 Sport, via Star)***

**CEBALLOS: SIRUDI MADRID**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), ameamua kuendelea kuichezea kwa mkopo Arsenal kuliko kurejea katika klabu yake ya nyumbani ya Real Madrid.***(AS, via Mirror)***

**LONGSTAFF AGOMBEWA ITALIA**

AC Milan na Inter Milan zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Newcastle United, Matty Longstaff (19). Nyota huyo anayeichezea Timu ya Taifa ya vijana ya England (U-20) anatarajia kumaliza mkataba wake na Magpies katika majira ya joto na mazungumzo kuhusu mkataba mpya yako kimya. ***(Times - subscription required)***

**CELTIC YAMTAKA WANYAMA**

TOTTENHAM imekubali kumruhusu kiungo wa Timu ya Taifa ya Kenya (Harambee Stars), Victor Wanyama kuondoka katika klabu hiyo lakini klabu inayomhitaji itatakiwa kulia ada ya pauni milioni nane. Celtic imeonyesha nia ya kumhitaji Mkenya huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# SERIKALI YATAKIWA KUWEKEZA KUWAIBUA SAMATTA 'WAPYA'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WABUNGE wameitaka serikali kuwekeza katika michezo ili kuwapata wachezaji wengine wazuri kama nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta ambaye hivi karibuni alisajiliwa na Aston Villa inayoshiriki Ligi Kuu England.

Samatta tayari ameanza kuitumikia timu yake hiyo mpya na Jumanne iliyopita alicheza mechi ya kwanza dhidi ya Leicester City na kupata ushindi wa mabao 2-1.

Wakiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, wabunge waliitaka serikali kuwekeza katika vifaa vya michezo na kuanzisha viwanja vya taaluma vya michezo.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Maulid Mtulia, alisema hivi sasa kuna mwamko mkubwa wa wazazi kutaka kushiriki katika michezo kutokana na kuchagizwa na mafanikio aliyoyapata Samatta.

"Lakini kuna tatizo kubwa la vifaa vya michezo, serikali ina mkakati gani kuhakikisha vifaa vinapatikana kwa urahisi," alihoji Mtulia.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Cecil Paresso, alisema Watanzania wengi kwa sasa wanamshangilia Samatta kwa kusajiliwa na timu hiyo ya England, lakini ni wazi amesajiliwa kutokana na jitihada zake binafsi.

"Hii inatuambia tunaweza kuwa na kina Samatta wengi kama serikali ikiwezeka vya kutosha katika michezo, kwa nini serikali isianzishe kwenye majiji makubwa 'sports arena'," alihoji.

Awali akijibu swali la Mbunge Mtulia, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, alikiri kuwapo na tatizo la vifaa vya michezo lakini wafanyabiashara wamekuwa wakihamasishwa kuagiza vifaa vya michezo kutoka nje ya nchi.

"Pia kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika viwanda vya kuchakata vifaa vya michezo," alisema Shonza.

Akijibu swali la Mbunge Paresso, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema kutokana na juhudi za serikali na wananchi wenyewe, sasa hivi Tanzania ina wachezaji 22 wanacheza soka la kulipwa na si Samatta peke yake.

"Tumeona vipaji havipatikani ukubwani, vinapatikana kwa kuanzia ututoni na ndio maana kuna michezo ya Umishumita kwenye shule ili kukuza vipaji,"



Wachezaji wa timu ya mpira wa Magongo, wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano mbalimbali watakayoshiriki kwenye Uwanja wa JKM Park jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA :JUMANNE JUMA**

# Tanzanite kamili kuwavaa Uganda

**Na Mwandishi Wetu, KAMPALA**

KIKOSI cha timu ya soka ya Taifa ya wanawake wa umri chini ya miaka 20 kinatarajia kuwakabili wenyeji Uganda katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia la Vijana utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa KCCA, Lugogo jijini Kampala.

Tanzania itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Januari 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema wamejiandaa vema kuwakabili wenyeji ambao wanafahamiana vizuri.

Shime alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa pande zote mbili, lakini akiwataka nyota wake kutulia na kulinda ushindi walioupata katika mechi ya kwanza.

"Tumejiandaa kupambana, ni mechi ngumu lakini sisi tuna faida ya ushindi tuliokuwa nao, mpaka sasa sisi tuko mbele, kikubwa ni kujiimarisha na kuongeza umakini, tutaingia uwanjani kwa tahadhari, wachezaji wote wanafahamiana na kila mmoja amejiandaa kupeperusha bendera ya nchi yake kwa heshima," alisema Shime.

Naye nahodha wa timu hiyo, Enekia Kasonga, alisema wako tayari kwa ajili ya kuwakabili Uganda na wamewataka Watanzania wasiwe na wasiwasi.

"Tumejiandaa vizuri, tumejipanga kwenda kumalizia kazi tuliyoianza, tunaamini hatutawaangusha," Kasonga alisema.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo atakutana na mshindi kati ya Senegal au Sierra Leone katika hatua inayofuata.

## Mkutano Mkuu Yanga wayeyuka

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Yanga umetangaza kuusogeza mbele mkutano mkuu wa dharura ambao awali ulitangazwa utafanyika Februari 16, mwaka huu kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jijini jana na Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, mkutano huo utafanyika katika siku nyingine itakayotangazwa hapo baadaye.

Msolla amewaomba radhi wanachama wa Yanga kwa mabadiliko hayo na kuwataka wawe na subira kwa ajili ya kuhudhuria mkutano huo utakapotangazwa tena. "Mkutano huo ulioitishwa kwa tangazo la Januari 28, mwaka huu, utaitishwa kwa tarehe nyingine itakayotangazwa hapo baadaye. Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza," Msolla alisema katika taarifa yake.

Moja ya ajenda zilizokuwa zinatarajiwa kujadiliwa katika mkutano huyo ni mapendekezo ya mabadiliko ya katiba yao.

## Azam FC yakiri Mtibwa kiboko

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Azam FC kikiwasili salama Iringa tayari kuwakabili Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Samora, uongozi wa timu hiyo ulikiri Mtibwa Sugar iliwasumbua.

Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema jana kuwa wanaenda Iringa kwa kazi moja ya kusaka ushindi ili kujiimarisha kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo linashikiliwa na Simba.

Iddi alisema kuwa wanasikitika katika mchezo huo watamkosa mshambuliaji wao Shabani Chilunda ambaye alionyeshwa kadi nyekundu katika mechi yao iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar.

**"Hatukuwa wazuri katika mechi yetu dhidi ya Mtibwa Sugar, mchezo ulikuwa na ushindani, magoli yalikuwa magumu kupatikana, lakini baada ya kumaliza mechi hii, tunaelekea Iringa kuwafuata Mbeya City, tutaendelea kupambana kama desturi yetu," Idd alisema.**


Baada ya mechi hiyo, Azam FC itarejea jijini Dar es Salaam kuwasubiri KMC katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru.

Michezo
Jumamosi Februari 1, 2020
Nipashe



## City yajitokeza kumwania Couto

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Leganes katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Mfalme iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nou Camp juzi usiku. Barca ilishinda mabao 5-0 na kusonga mbele katika michuano hiyo. PICHA: MTANDAO

# SIMBA, COASTAL UNION KIBARUANI

## Wagosi wa Kaya watamba wamejipanga kufuta 'uteja' dhidi ya vinara hao wa Ligi Kuu...

**Na Somoe Ng'itu**

HAWATOKI! Hayo ni maneno kutoka kila upande kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya mabingwa watetezi, Simba dhidi ya wageni Coastal Union inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili jana kikosi chao kimejipanga vizuri kuendelea kujiimarisha katika mbio za ubingwa kwa kupata pointi tatu muhimu katika mechi hiyo.

Matola alisema hata hivyo wataingia uwanjani wakiiheshimu Coastal Union na hawatabweteka kutokana na kumbukumbu ya kupata ushindi mnono katika mechi yao ya msimu uliopita, ambapo Simba ilitoa kichapo cha bila huruma cha mabao 8-1.

"Tumeendelea na mazoezi kama kawaida, hakuna mechi rahisi, na kila mmoja anataka kupata ushindi, hatutawadharau Coastal Union, timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu zimejipanga na zinahitaji ushindi, tunasisitiza kila mechi kwetu ni fainali," Matola alisema.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba alisema wataongeza nidhamu na wamewakumbusha nyota wao kuongeza utulivu ili kutumia vema nafasi watakazozitengeneza.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili timu yake imejipanga vema kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi hiyo licha ya kuwa na historia ya kufungwa na Simba kila wanapokutana.

Mgunda alisema kuwa maandalizi waliyofanya ni ya kukutana na Simba katika msimu huu, na kamwe hawataingia uwanjani na kumbukumbu ya mchezo uliopita ambao walipoteza kwa kichapo cha mabao 8-1.

"Kikubwa tumejiandaa vizuri, itakuwa ni mechi yenye ushindani, tunajua tutacheza na timu nzuri, ndio wenye uongozi kwenye ligi yetu, kubwa tumejipanga kwenda kupambana nayo, historia ina mantiki yake, lakini tumejiandaa kwa ajili ya msimu huu," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema ameimarisha kikosi chake kwa kusajili wachezaji wapya wawili katika dirisha dogo, mlinzi wa kati, Hans Masoud na kiungo mshambuliaji, Hamad Majimengi ambao anaamini watawasaidia kufikia malengo yao.

"Filosofia yetu sisi Coastal Union ni kutumia wachezaji vijana, ninaamini watatusaidia kufika tunapopahitaji katika msimu huu," Mgunda aliongeza.

Naye mshambuliaji Haji Ugando alisema Simba wasitarajie mteremko katika mechi hiyo kwa sababu msimu huu timu yao imeimarika zaidi na itaingia uwanjani ikiwa tofauti.

"Mechi hii tumejiandaa vema, Simba wategemee watakutana na ushindani wa kutosha, kwa sababu tumejipanga na tuna kumbukumbu ya kufungwa magoli nane, wasiichukulie mechi kama ilivyokuwa iliyopita," Ugando, mchezaji wa zamani wa Simba alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma ni kati ya Tanzania Prisons dhidi ya KMC FC wakati kesho Yanga itawakaribisha Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Taifa.

## Samatta mzigoni England tena leo

**LONDON, England**

MASHABIKI wa soka wa nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wanatarajia leo kukusanyika katika maeneo mbalimbali nchini kumshuhudia nyota wao, Mbwana Samatta, akicheza mechi yake ya pili baada ya kusajiliwa na Aston Villa wiki iliyopita.

Mechi ya ugenini dhidi ya AFC Bournemouth itakuwa ni ya pili kwa Samatta tangu ajiunge na Aston Villa endapo atapangwa, lakini utakuwa ni mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu England kwa mshambuliaji huyo aliyetua klabuni hapo kwa dau la pauni milioni 8.5.

**Kocha wa Bournemouth, Eddie Howe anatarajiwa kuwatumia nyota wake waliokuwa majeruhi , Jefferson Lerma na Diego Rico kuikabili Aston Villa licha ya kuendelea kuwakosa wachezaji wengine muhimu akiwamo mshambuliaji, Joshua King ambaye anawindwa na Manchester United.**

Villa inatakiwa kuweka nguvu zaidi ya kupata ushindi katika mechi za Ligi Kuu England na kujiondoa kwenye mstari wa kushuka daraja ambao unazihusisha timu sita na kuacha kufikiria fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Machi Mosi mwaka huu kwenye Uwanja wa Wembley.

Bournemouth yenyewe ilishatolewa kwenye michuano hiyo na Arsenal wakati Villa wao waliwaondoa Leicester.

Wenyeji wamevuna pointi 18 kwenye uwanja wao wa nyumbani katika mechi 18 walizocheza wakati Villa imeshinda mchezo mmoja tu wa ugenini kati ya michezo 10 za ugenini ikiwamo sare dhidi ya Brighton.

Baadhi ya mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Liverpool dhidi ya Southampton wakati Leicester City watakaribisha Chelsea huku Manchester United ikiwavaa Wolves na West Ham itacheza na Brighton.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >